# *MUNGU WA WAKATI HUU MWOVU*

. . .yatendeka, amini tu;
Amini tu, amini tu,

Na tuinamishe vichwa vyetu. Baba mpenzi wa Mbinguni, tunashukuru asubuhi ya leo ya kwamba tunaweza kuamini. Imewezekana kwa Damu iliyomwagika ya Mwanao, Yesu, ya kwamba tungekuwa washiriki wa neema Yake; na kufanyika wana na binti za Mungu, kwa utii Wake hata mauti pale msalabani, tunahesabiwa haki kwa kumwamini Yeye na kufufuka Kwake, na sasa Roho Mtakatifu amemwagwa mioyoni mwetu.

2 Tunashukuru kwa ajili ya nafasi hii ya kuja hapa asubuhi ya leo kushiriki mawazo yetu na kukuabudu kwetu, kujieleza kwa nyimbo, shuhuda, kusoma Zaburi, kusoma Neno Lako, na kumngojea Roho Mtakatifu kwa uchaji kutuletea Ujumbe uliokusudiwa kwa ajili ya saa hii. Tujalie, Bwana. Tujalie kufaidika kwa kuwapo mahali hapa leo. Na tutakapoondoka kwenye jengo hili, na tuseme kama wale waliotoka Emau, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi asubuhi ya leo?" Tujalie mambo haya, Mungu wa Milele, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ketini.

3 Habari za asubuhi, marafiki, hapa, hapa nje maskanini na kwa marafiki wetu kila mahali nchini, kote kote kutoka Pwani ya magharibi, tena asubuhi ya leo, hadi Pwani ya Mashariki, na kaskazini na kusini, kwenye mawasiliano ya simu.

4 Ni siku nzuri hapa Indiana, kidogo, kuna mawingu kidogo, kumepoa, kuzuri sana. Maskani imejaa watu, huko nje uani na kuzunguka kuta. Tuna matarajio makubwa sana ya Bwana kutuzuru leo. Nasi tunatumaini ya kwamba Mungu amewapa siku njema po pote mlipo. Na ni siku njema, kwa maana Bwana ameitoa. Haidhuru hali ya hewa ikoje, ni siku njema. Tuna furaha kuwa hapa, tungali na furaha ya kwamba tuna nafasi ya kuuelezea ulimwengu imani yetu katika Yesu Kristo. Nasi tunataka kuchukua kila nafasi tuwezayo kuchukua kuonyesha matendo yote ya upendo Wake na yale aliyotufanyia. Leo sisi tuna. . .

5 Nilipewa, muda mfupi uliopita, ta—tangazo la kutangaza, halafu nina mambo machache hapa ningetaka kusema. Na moja ya hayo, nilipewa tangazo kuhusu mkutano wa halmashauri kwenye usiku wa juzi. Na kulikuwa na shemasi mmoja kutoka

kanisani ambaye amehamia Arizona, ambaye ni Ndugu Collins, ndugu yetu mpendwa. Na wakati hayuko, wao, ile halmashauri, imemchagua Ndugu Charlie Cox kuchukua mahali pake wakati ameondoka. Na Ndugu Charlie Cox amechaguliwa rasmi na wadhamini . . . ama halmashauri ya mashemasi ya kanisa hili, kuchukua kazi ya Ndugu Collins, wakati hayupo.

6 Na jambo ninalotaka kusema, tena, ninataka kuwashukuru ninyi nyote, maana wengine wenu huenda wakaenda nyumbani kabla ya ibada ya uponyi usiku wa leo, kwa ajili ya vizawadi vidogo vizuri, upendo. Tumeletewa chakula kingi tangu tumekuwa hapa. Na kutoka kwangu na kwa mke wangu, na familia yangu, kweli tulifurahia jambo hilo. Wakati mwingine mimi husahau hata kusema lo lote juu ya jambo hilo. Nina shughuli nyingi sana, mwajua. Akili yangu daima ininazunguka sana. Mnaweza kuwazia ni kitu gani, juu ya watu, si kutoka tu kutoka papa hapa kwenye kanisa hili, bali kutoka kila mahali duniani. Mnaona? Na kwa namna fulani jambo hilo linakuweka daima katika fadhaa.

7 Mtu fulani alikuwa akizungumza juu ya kuweka watoto wakfu, na ibada za ubatizo, na kadhalika. Hilo ni jambo zuri sana. Laiti ningaliweza kufanya jambo hilo, lakini linatatiza sana, ni—ni vigumu kwangu kupata wakati. Sina budi kuweka nia yangu moja kwa moja kwenye jambo hili, Ujumbe huu. Mnajua Biblia iliwaambia wale mitume, ama . . . Wale mitume, hasa, katika Biblia, walisema, "Nendeni makatafute, miongoni mwenu, watu wenye sifa njema, na watu waaminifu na waliojazwa na Roho Mtakatifu, ili kwamba wayashughulikie hayo mambo." Nami nilimwambia Billy . . .

Yeye alisema, "Unaenda kumweka wakfu yule mtoto mchanga wakati huu, baba?"

Nikasema, "Lo, jamani!" Mnaona? Kama . . . Tuna wengi wao wanaongoja kuwekwa wakfu, na hiyo ni kweli, itanibidi tu kurudi na kuchukua siku maalum kwa ajili ya kuweka watoto wachanga wakfu. Kwa hiyo ningetaka kufanya jambo hilo, sasa.

8 Lakini tunataka kuwashukuru kila mmoja wenu kutoka mioyoni mwetu; mimi, mke wangu mimi, na jamaa yetu. Watu wanatuletea chakula cha mikebe, njugu-siagi, tikiti, tikitimaji, loo, maforsadi. Kila kitu tu kinachoweza kuwaziwa, wao wanakileta.

9 Ndugu fulani wa thamani na dada yake, juzijuzi, walituletea bata mzinga mnene. Ningali ninamla. Na kwa hiyo ninii tu . . . Loo, nami sina budi kummaliza kabla sijaondoka, nadhani. Kwa hiyo kama simmalizi, mke wangu atambeba twende naye. Na kwa hiyo—kwa hiyo tutaninii . . . Bila shaka tunafurahia mambo haya. Najua wengi wa watu hawa; wengine wao siwajui. Wao watakuwa wamekaa ukumbini tutakapoingia. Na kwa hiyo bila shaka ninathamini jambo hilo.

Na wengi ninajua nimepata . . . Nimewaona wengi, na kuna wengi ambao sipati kuwaona. Ni—nina hakika kila mtu anafahamu ya kwamba ni—ningetaka kumfikia kila mtu niwezaye, lakini mimi ni mmoja tu. Mnaona? Ku- . . . Siwezi kumfikia kila mtu. Ninafanya kila nijualo la kufanya.

10 Kwa hiyo, Mungu awe pamoja nanyi. Nina hakika ya kwamba kuna Mmoja atakayekuwa pamoja nanyi; huyo ni Yesu Kristo, na Yeye anaweza kuwa pamoja nanyi. Yeye ndiye Mtu pekee aliyepo kila mahali. Naye pia ana nguvu zote, kwa hiyo anaweza kuwapeni kila haja. Na anajua yote, pia, na anajua haja zenu, za yale mnayohitaji.

11 Ninamwamuru kila mmoja ambaye sitaninii . . . Nimekuwa nikifanya haraka niwezavyo, hata tangu nimekuwa hapa asubuhi ya leo, nami nitamfikia kila niwezaye kumfikia. Na endapo . . . Jambo ninalokosa, Mungu aliye mwenye nguvu zote ata—atawapeni kila mnachotaka kadiri ya utajiri Wake katika Utukufu.

12 [Ndugu Branham anakoma, kisha anazungumza na Ndugu Neville.] Siwezi kuona huo vizuri sana. Unaweza kusoma?

Ni tangazo maalum la namna fulani. Nami nafikiri hapana budi Billy Paul aliliandika. Kwa hiyo yeye ni kama mimi; siwezi hata kusoma mwandiko wangu mwenyewe. Na kwa hiyo nina mwandiko wangu mwenyewe wa mkato. Na kama mngaliona baadhi ya maandiko yangu hapa, yaliyoandikwa hapa, mnafikiri mngaliyaelewa hayo? [Ndugu Branham analionyesha kusanyiko maandiko yake, na anacheka pamoja nao—Mh.] Nina kitu kama nyota, inavuka daraja, na kadhalika, yote tu.

[Ndugu Neville anasoma tangazo—Mh.]

Ndugu Adair, Adair wa Arkansas, amwone Kasisi Pearry Green huko nyuma ya kanisa mara moja. Vema.

13 Sasa, kwa hiyo jambo lingine ambalo ninge—ningetaka kutangaza hapa ni—ni kwamba, usiku wa leo sasa kwa ajili ya ibada za uponyaji. Tutawaombea wagonjwa usiku wa leo, na kwa hiyo na—natumaini ya kwamba mtakuwa hapa.

14 Sasa tunawapelekea salamu watu wote kila mahali nchini, katika Jina la Bwana Yesu, ili kwamba Mungu awabariki asubuhi ya leo. Wengine wenu wanakaribia saa sita. Huko New York, ni karibu saa sita. Na huko Arizona, Pwani ya Magharibi, ni kama tu saa moja. Kwa hiyo kuna . . . Na hapa tuko moja kwa moja katikati. Kwa hiyo Mungu awabriki mnaposikiliza. Sasa hili laweza kuwa . . .

Nimeamua moyoni mwangu, wakati tuko hapa . . .

15 Na hatukuruhusiwa kukodisha jumba la mikutano, na hatimaye kwa namna fulani wakaturuhusu; tungeweza kufanya ibada moja, ila hatupaswi kuwaombea wagonjwa. Mimi—mimi sininii . . . Hiyo ndiyo huduma yangu. Sina budi kufanya yale

Roho Mtakatifu anayonimbia nifanye. Kwa hiyo ni—nilikataa, kwa sababu ninataka kuwa huru kufanya lo lote Roho Mtakatifu asemalo nifanye. Mnaona? Kwa hiyo nikawazia tunaweza tu kuvumilia siku moja zaidi, hata hivyo, hapa Maskanini. Kumepoa asubuhi ya leo. Bwana ametuandalia siku nzuri tu hapa, kwa hiyo tunashukuru.

16 Sasa, katika kufanya jambo hili, nimekuja hapa kwa kusudi la kufundisha vile Vitasa vya mwisho, vile Vitasa Saba vya mwisho, na Baragumu Saba za mwisho, na Ngurumo Saba za mwisho, za Kitabu cha Ufunuo, kuzifungamanisha pamoja katika saa hii tunayoishi sasa; kufuata kule kufunguliwa kwa zile Muhuri Saba, Nyakati Saba za Kanisa. Kwa hiyo, hatukuweza kupata nafasi kufanya jambo hilo. Kwa hiyo na—natumaini ya kwamba, mara niwezapo, tuta-. . . tunapoweza kupata mahali panapotosha kwa jambo hilo, aidha hapa ama Louisville, New Albany, ama aidha kupiga hema, ili tuweze tu kukaa muda ambao Bwana atatuongoza kukaa.

17 Lakini katika jambo hili sasa, nilichukua nafasi hii kuwaeleza watu wazo langu na imani yangu katika Mungu, kisha kuwaleta kwenye saa tunaoyoishi. Na kwa jambo hili, halielekezwi kwa mtu ye yote yule, kanuni za imani, cho chote kile; ni kama tu ninavyoona Neno la Mungu. Na Jumapili iliyopita tulikuwa na kumiminiwa kwa wingi sana kwa Roho juu ya Neno. Ulikuwa mrefu sana, nami nilichukia kukaa muda huo wote; lakini hata hivyo hatujui ni wakati gani tutakaokutana kwa mara yetu ya mwisho. Nasi hatuna budi, kama . . . tunavyotaka kuwa. Ninataka kuwa, hasa, kama Paulo wa zamani alivyosema, "Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya Kusudi lote la Mungu." Yesu alisema hakuwaficha kitu wanafunzi Wake.

Na kama vile mimi, nikiwa na shughuli nyingi kujaribu kudumu chini ya upako wa Roho Mtakatifu, kutaka kujua ni—ni saa ngapi, Ujumbe wa wakati huu, wakati mwingine mimi hushindwa kutoka nje na kufanya wajibu wangu kama mtumishi wa Kristo, kama mhudumu. Lakini nina watu wengi wanaojaribu kunisaidia kufanya jambo hili, nami nashukuru kwa jambo hilo, ndugu zangu wote wahudumu.

18 Sasa, simaanishi kujaribu kuwaweka watu. Kama ninyi, huko nje nchini ambako Ujumbe unaenda, mngeweza kusimama na kuangalia kila mahali humu kanisani asubuhi ya leo, kwenye marefu ya kanisa, vyumba vya watoto wachanga, huko nje, redio zimefunguliwa, kwenye mabasi, matrela, na kadhalika, na motokaa, mngeweza kuona shida ni nini. Halafu basi kila ibada, wengi, wengi wakipita kwa magari; wakipiga simu, na kadhalika, hawangeweza kuja, karibu na hapa. Nasi tunahitaji nafasi kubwa ili watu waweze kuketi na kustarehe.

Halafu kuleta U—Ujumbe ambao ninafikiri ni muhimu sana, najisikia kwamba inatupasa, kila mmoja, tujisikie vizuri tukiwa tumeketi, ili kwamba tuweze kusikiliza; tukiwa na penseli zetu na karatasi, na mihitasari na Biblia, na kadhalika, kuandika mi—mihitasari. Lakini kwa njia hii nilifikiri ningerudi nyuma kwenye wakati tulio nao, tunaoishi, na kujaribu kuleta baadhi ya mambo haya ambayo mtakabiliana nayo. Nanyi mtayahitaji.

19 Kama nikija hapa leo, ama siku yo yote ile, ama mhudumu mwingine ye yote, kujaribu kuleta ujumbe kwa watu, watu wanaokufa kama sisi, na wakati umekaribia sana, kama ninavyoamini kwa siku hii; ningekuwa mnafiki kujaribu kuleta kitu ambacho ninajua ya kwamba mngekifurahia na kingekuwa dhidi ya Neno la Mungu, ama kitu fulani kuvutia umati wa watu, ama—ama kitu kama hicho; ni—nisingekuwa . . . nisingekuwa kile ni—nilicho hapa kuwa, mtumishi wa Kristo. Ninataka kuleta kitu ninachofikiri ni muhimu sana kwenu, si kuonwa tu; bali kufikiri ni kitu ambacho kama nikifa leo, kesho kitatiwa nanga moyoni mwenu kuendelea mbele na kumtumikia Mungu.

20 Sasa nataka kusema ya kwamba kuna kitu kilicho karibu kutukia. Ninajua jambo hilo. Wengi wenu hapa mnakumbuka wakati Ndugu Junior Jackson alipokuja kwangu punde tu kabla sijaelekea Arizona, juu ya ndoto aliyopata. Jambo la ajabu! Ni wangapi wanaokumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naye Bwana akatupa fasiri yake, nalo likatukia kikamilifu. Sasa, ndio kwanza apate ndoto nyingine, kitu fulani.

21 Na jambo la ajabu, mtu fulani alikuwa hapa juzijuzi, kutoka Oregon. Ni vigumu kwake kunijua, naye alikuwa . . . aliota ndoto ile ile juzijuzi, ambayo Junior Jackson aliota, na—na akaja akaniambia. Si—sijui tafsiri yake; ninamngojea Bwana. Lakini ninajua itakuwa ni kitu fulani kinachokuja kutoka kwa Mungu. Kumbukeni tu jambo hilo. Ni BWANA ASEMA HIVI. Ni kitu fulani kinachokuja kutoka kwa Mungu. Sijui ni kitu gani. Ni ajabu kweli, ajabu sana! Kwa kweli, kulingana na zile—zile ndoto ambazo hao watu wawili . . . Mmoja wao ninge- . . . huenda akawa ni Mbatisti, Mpresbiteri. Hu—huenda ameketi hapa asubuhi ya leo. Sijui. Alikuwa hapa juzijuzi, simjui mtu huyo.

22 Lakini aliisimulia ile ndoto, akiwa na machozi machoni mwake. Nayo ilimtetemesha. Yeye alitoka huko kote Oregon mpaka hapa, kuisimulia. Ndugu Jackson alikuja jinsi ile ile, asubuhi ya leo. Mtu mmoja akiwa hamjui mwingine; mmoja, maelfu ya maili kutoka kwa mwingine, na ndoto zote mbili juu ya kitu kile kile kabisa. Kwa hiyo Roho Mtakatifu anaishikilia fasiri yake nisiijue. Sijui nimwambie nini mtu huyo. Lakini ninajua Mungu anajitayarisha kufanya jambo fulani, nalo litakuwa tukufu machoni petu.

23 Sasa, Ujumbe asubuhi ya leo, ninataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Wagalatia. Mimi sihubiri ama kuninii... Ni somo la shule ya Jumapili. Na sasa, ninyi wanaume na wanawake ambao mnasimama karibu na kuta, na mtu fulani anataka kubadilishana na kuketi kidogo, ama cho chote kile, sasa, hamtanisumbua; iweni tu na kicho. Na iwapo akina mama, watoto wao wanalia ama cho chote kile, mtu fulani atatoka kwenye chumba cha watoto wachanga ili kwamba wapate nafasi kwa ajili ya huyo mtoto mchanga.

24 Na sasa chukueni penseli zenu, Biblia, na mwe tayari kuandika Maandiko machache ambayo tutasoma. Sitaki mjisikie mmefungwa. Nawatakeni mjisikie—nawatakeni mjisikie huru kuketi na kusoma. Na huenda msikubaliane, ambalo ni sawa. Lakini ninazungumzia jambo hili kwa nchi nzima asubuhi ya leo, ili kwamba watu ambao wameamini Ujumbe ambao Bwana Yesu amenipa kwa ajili ya wakati huu, wapate kujua yale yanayotendeka, na kuyaweka kwenye Maandiko.

25 Jumapili iliyopita tulinena juu ya *Watiwa Mafuta Katika Siku Za Mwisho*. Na iwapo ninyi, ye yote wenu, ni wasikilizaji wa kanda, hakikisheni mmepata kanda hiyo. Si kwamba tunataka kuuza kanda; hiyo siyo nia. Nia ni kuupeleka Ujumbe nje. Mnaona? Mnaona? Kama una kinasasauti, kusanya kundi la watu pamoja, ukaicheze, na msikilize kwa makini. "Watiwa Mafuta."

26 Mnawasikia watu wakiinuka na kusema, "Loo! Biblia ilisema, 'Katika siku za mwisho, manabii wa uongo watainuka na kufanya ishara hizi.'" Hayo ni Maandiko hasa. Basi hayo yako mahali gani? Halina budi kutumiwa vizuri.

Usiku wa leo ninataka kunena juu ya, Bwana akipenda, juu ya: *Mungu Akifunuliwa Katika Neno Lake Mwenyewe*, jinsi ambavyo jicho haliwezi kuwekwa mahali sikio linapaswa kuwa. Mnaona? Ni kama tu kuchapishwa kwa Biblia nzima, na, katika Biblia nzima, humwonyesha Yesu Kristo. Kwa hiyo ninataka kunena juu ya jambo hilo usiku wa leo, Bwana akipenda. Na sasa, kama sivyo, tarehe fulani baadaye.

27 Sasa katika Kitabu cha Wagalatia. Na katika Kitabu cha Wakorintho wa Pili 4:1 mpaka 6, halafu Wagalatia 1:1 mpaka 4, ninataka kusoma Maandiko fulani. Sasa Katika Wagalatia 1:1 mpaka 4, "Paulo, mtume," angalia kule kusimama upesi sana. *Mtume* maana yake ni "mtu aliyetumwa," ama, "mmishenari."

> *Paulo, mtume (si mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali...Yesu Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu,)*
>
> *Na ndugu wote walio pamoja nami, kwa makanisa ya Galatia;*

*Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo;*

*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu.*

*Utukufu una yeye milele na milele. Amina.*

28 Sasa katika Kitabu cha Wakorintho wa Pili, sura ya 4, na tutasoma kutoka aya ya 1 mpaka aya ya 6.

*Kwa sababu hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivypata rehema, hatulegei;*

*Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyosiririka, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichangaya neno la Mungua na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu.*

*Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea*;

Kama hilo halileti kuchaguliwa tangu zamani, sijui ni kitu gani kinakuleta.

*Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.*

Kama ilivyokuwa katika Bustani ya Edeni, "Wafukuze, wasije wakagusa ule Mti."

*Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana*;. . .*sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya* Kristo.

*Kwa kuwa Mungu, aliyesema Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu*,na *atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo*.

29 Amina! Neno linasema hivyo! Sasa, somo langu asubuhi ya leo, ni: *Mungu wa Wakati Huu Mwovu*. Kama tulivyosoma kwenye Maandiko, "mungu wa dunia hii, wakati huu mwovu." Sasa, Ujumbe huu unaonyesha maovu ya wakati huu mwovu, na unfaa kwa kutabiri kwa wakati huu mwovu.

Nami ninaamini ya kwamba kila. . .ya kwamba Biblia ina kila jibu kwa ajili ya kila kizazi, tayari limeandikwa kwenye Biblia, kwa ajili ya mwamini wa wakati huo. Ninaamini ya kwamba kila kitu tunachohitaji kimeandikwa papa *Hapa*, kinahitaji tu kufasiriwa na Roho Mtakatifu. Siamini ya kwamba mtu ye yote duniani ana haki ya kuweka fasiri yake kwenye Neno. Mungu hahitaji mtu ye yote kulifasiri Neno Lake. Yeye ndiye anayejifasiria. Alisema angefanya jambo hilo, Naye hulifanya.

30 Kama nilivyosema mara nyingi. Alisema, "Bikira atachukua mimba," alinena hayo kwa kinywa cha nabii, naye akachukua mimba. Hakuna mtu anayepasa kufasiri jambo Hilo. Hapo mwanzo, Yeye alisema, "Iwe nuru," ikawa. Hakuna mtu aliyepaswa kufasiri jambo Hilo. Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, Yeye angeimwaga Roho Yake juu ya watu wote," Naye akaimwaga. Halihitaji ye yote alifasiri. Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, mambo haya," tunayoyaona yakitukia sasa, yangekuwa hapa. Halihitaji kufasiriwa kwo kwote. Tayari limefasiriwa. Mnaona?

31 Sasa, angalieni kwa makini sasa tunapolisoma Neno. *Mungu Wa Wakati Huu Mwovu*, tunakoishi sasa. Laweza kuonekana la kushangaza, jambo la kushangaza sana, katika wakati huu wa neema, wakati, "Mungu anatwaa watu kwa ajili ya Jina Lake," hiyo ni kusema, Bibi-arusi Wake, katika wakati huu mwovu unaopaswa kuitwa wakati wa maovu. Wakati ule ule ambao "Mungu anawaita watu kwa ajili ya Jina Lake," kwa neema, watoke, na unaitwa wakati mwovu. Sasa, tutathibitisha kwa Biblia ya kwamba huu ndio wakati ambao Yeye alikuwa akinena habari zake. Ni jambo la ajabu sana kuwazia hilo, ya kwamba katika wakati mwovu kama huu, ya kwamba Mungu wakati huo angekuwa anamwita Bibi-arusi Wake.

32 Hivi mlitambua, Yeye alisema, "watu," si "kanisa." Kwa nini? Hata hivyo, linaitwa Kanisa, lakini Yeye angewaita "watu." Sasa, kanisa ni kusanyiko la watu wengi wa matabaka mbalimbali, bali Mungu anamwita Mmoja hapa. Yeye hakusema, "Nitawaita Wamethodisti, Wabatisti, Wapentekoste." Alisema angewaita watu. Kwa ajili gani? Jina Lake. Mnaona, watu; mmoja kutoka kwenye la Methodisti, mmoja kutoka kwa la Kibatisti, mmoja kutoka la Kiluteri, mmoja kutoka kwa la Katoliki. Mnaona?

Lakini yeye anaita, si kundi la kanisa, bali "watu kwa ajili ya Jina Lake," ambao wanalipokea Jina Lake, wameposwa katika Jina Lake, wanaokwenda arusini kuolewa Naye, kuwa sehemu Yake, kwa kuchaguliwa tangu zamani. Ni kama tu mwanamume anayechagua mke mzuri maishani, aliyechaguliwa kuwa sehemu ya mwili wake. Kwa hiyo, hiyo ni kusema, Bibi-arusi wa Kristo atakuwa, na sasa ameninii, tangu zamani, amechaguliwa na Mungu kuwa sehemu ya Mwili huo. Mnaona? Lo! Maandiko yamekolea sana, yamejaa asali!

33 Angalia, si kile mtu fulani amesema, wala mtu fulani alioita; bali ni wale waliochaguliwa na Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, naye anawaita watu hawa katika siku za mwisho; si madhehebu. "Watu kwa ajili ya Jina Lake." Na wakati huu mwovu ndipo Yeye anafanya jambo hilo, wakati uu huu wa undanganyifu.

34 Juma lililopita, katika Mathayo 24, ulikuwa ndio wakati mdanganyifu sana kuliko nyakati zote. Nyakati zote za udanganyifu, tangu bustani ya Edeni, kote kote, hakujakuwa na wakati wa udanganyifu kama wakati huu. “Manabii wa uongo watainuka na kuonyessha ishara na maajabu, kama yamkini kuwapoteza hata walio Wateule.” Mnaona? Sasa, makanisa tu baridi, ya kawaida, magumu, na kadhalika, ya theolojia za kujitengenezea, hayo hayangeweza; walio Wateule wasingewajali. Lakini ni kule juu karibu sana na jambo lililo halisi. Kuacha tu Neno moja ndivyo tu unavyopaswa kufanya. Lililoahidiwa kwa wakati huu; wakati mkuu sana! Enyi Wakristo, kila mahali, jihadharini na saa tunayoishi! Andikeni, na someni, na msikilize kwa makini.

35 Ni kwa nini Mungu angewaita watu kwenye wakati huu mwovu, kwa ajili ya Jina Lake? Sababu yake ni kwamba, ni kumjaribu Yeye, Bibi-arusi Wake. Ni ku-. . . Wakati amedhihirishwa, akajaribiwa, kuthibitishwa, akathibitishwa kwa Shetani. Kama ilivyokuwa hapo mwanzo, hivyo ndivyo itakavyokuwa hapo mwisho.

36 Kama mbegu inavyoanza ardhini, inapitia kwenye wabebaji, uhai wake, lakini inaishia katika mbegu ile ile iloyokuwa wakati ilipoingia ardhini.

Na jinsi vile vile mbegu ya udanganyifu ilivyoanguka ardhini, katika Edeni, ndivyo inavyoishia katika siku za mwisho.

Kama tu vile Injili ilivyokuwa wakati ilipoanguka katika madhehebu huko Nikea, Rumi, inaishia katika madhehebu supa.

Kama tu vile Mbegu ya Kanisa ilivyoanguka huko nyuma, ikiwa na ishara, maajabu, na Kristo aliye hai miongoni mwao, inaishia katika siku za mwisho chini ya huduma ya Malaki 4, na kuirudisha tena Imani asili iliyotolewa mara moja.

37 Tunaona sasa, wakati huu mwovu ni kuthibitisha, kwa Shetani, Yeye si kama Hawa, ya kwamba Yeye si mwanamke wa namna hiyo. Naye atajaribiwa kwa Neno Lake, Bibi-arusi, kama bibi-arusi wa Adamu alivyojaribiwa kwa Neno. Na bibi-arusi wa Adamu aliamini kila sehemu ya Neno, lote, ila akachanganyikiwa kwenye ahadi moja, ya kwamba, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” leo; Lakini akashindwa kwenye ahadi moja, kwa kujaribiwa na adui, uso kwa uso. Na sasa, watu wanaoitwa kwa ajili ya Jina Lake, bila shaka, ni Bibi-arusi Wake. Yeye atakutana tena na jambo lile lile; si kwa kweli tu ya kimadhehebu au kitu fulani, bali kila Neno!

38 Kwa sababu, katika mwanzo wa Biblia, mwanadamu alipewa Neno la Mungu apate kuishi kwalo. Neno moja, likafasiriwa vibaya na m—mtu aliyeitwa Shetani, katika utu wa mnyama aliyeitwa nyoka. Shetani, katika mtu huyu, angeweza

kuzungumza na Hawa, na kumfasiria vibaya Neno, kisha akapotea. Mnaona, haina budi kuwa ni kila Neno.

39 Katikati ya Biblia, Yesu alikuja akasema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno," wakati alipojaribiwa na Shetani.

Sasa, Mungu akitwambia hapa katika siku za mwisho, ya kwamba, "Mungu wa dunia hii atainuka katika siku za mwisho."

"Na mtu ye yote atakayeongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima."

Mungu aturehemu! Na tusitembee kama wenye majivuno, vifua mbele, kichwa juu, wajuvi, kwa maana sisi pia wakati mmoja tulikuwa katika kuasi. Hebu kwa neema, na rehema, na kujisikia moyoni mwetu kwa Mungu, tuje kwa unyenyekevu kwenye Kiti cha Enzi cha neema.

40 Ajabu sasa, baada ya miaka elfu moja mia tisa ya kuhubiriwa kwa Injili, na sasa huo, yaani utaratibu wa ulimwengu, ni mwovu zaidi kuliko siku ambazo yule, wakati Yeye alipokuwa hapa. Utaratibu wa ulimwengu ni mwovu zaidi. Ulimwengu unaelekea kwenye upeo mkuu. Mnajua jambo hilo. Bwana anatimiza Neno Lake kwa kila njia.

41 Jana, nikisimama. . .Natumaini jamaa mdogo hataninii. . . Hatafanya hivyo. Nilikuwa nimekuja na mke wangu, na Bibi Woods, Ndugu Roy Roberson, mahali fulani hapa, Ndugu Woods, tulikuwa tumesimama hapa kwenye Kituo hiki cha Maduka ya Youngstown, kuchukua ki—kifurushi alichokuwa nacho Dada Woods. Na kwenye. . .tulipokuwa tumesimama pale, jamaa mdogo akaja na kujitambulisha mwenyewe, na simjui. Kijana mwingine akaja akasema walitoka aidha Alabama, Georg-. . . Ninaamini Georgia, maana niliwauliza kama walimjua Ndugu Welch Evans. Nasi tukazungumza dakika chache. Na wakati nilipoanza kuodoka, mvulana huyu mdogo alinitazama. Wakati yule kijana mwingine na mvulana wake mdogo walipoondoka, kijana huyu mdogo aliniangalia. Akasema, "Ningetaka kusema jambo moja tu."

Nikasema, "Hivi wewe—wewe ni mwamini? Wewe ni Mkristo?"

Akasema, "La, bwana." akasema, "Nime-. . . "

42 Huenda nisinukuu neno alilosema hapa, lakini huenda alikuwa kidogo anatilia shaka. Nilikuwa nimemuliza kuhusu kule kutokea kwa Malaika wa Bwana. Naye akasema alikuwa amesikia habari hiyo, lakini yeye hajakuwa kanisani hapo awali, kanisa hili. Nikasema, "Hivi unaamini jambo Hilo?"

Kasema, "Naam, bwana." Akasema, "Ni—nimekuwa nikiangalia jambo fulani." Kasema, "Watu wamekuwa wakiniambia juu ya nabii hizi na kadhalika, nami nikasikia

kwenye kanda ya kwamba ulitabiri jinsi California ingepasuka namna hiyo." Kisha akasema, "Nilipoona jambo hilo gazetini, basi nikaamini." Akasema, "Nitakuja leo ama kesho," hiyo ni leo, "kwa mara yangu ya kwanza."

Nikasema, "Bwana akubariki, mwanangu," na nikaanza kumpa mkono.

Akasema, "Lakini ninataka kukwambia jambo fulani, bwana." Akasema, "Mimi nimepotea kabisa." Akasema, "Mimi ni kama sarafu kwenye lundo la mchanga, nimepotea!"

43 Nikasema, "Lakini haikubidi kukaa hivyo. Kuna Mtu fulani anayesimama hapa sasa ambaye anaweza kukupata wakati wo wote ambapo upo tayari kupatikana."

Akasema, "Niko tayari."

Nikasema, "Unaweza kuinamisha kichwa chako?"

Akasema, "Mimi sioni haya."

Si hivyo tu, lakini alipiga magoti, pale katika mahali hapo pa kuegeshea magari, mbele ya watu wote. Watu barabarani wakimwangalia. Pale tukaomba pamoja naye, mpaka akamtolea Mungu moyo wake. Alikuja, akiwa mwenye dhambi; akarudi, akiwa mwana wa Mungu. Alienda karibu na motokaa, amekufa; akarudi, akiwa hai.

44 Nikasema, "Kidimbwi kitafunguliwa kesho."

Damu imebubujika,
Ni ya Imanueli,
Wakioga wenye taka,
Husafiwa kweli.

Nikasema, "Inuka ukabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, ukiliita Jina la Bwana. Mungu atakujaza na Roho Mtakatifu, na kukupa mambo haya makuu, na kukufanya uweze kuona jambo Hilo."

45 Ni kitu gani? Ulimwengu unaelekea kwenye upeo. Kwa nini? Roho ya kuasi, utovu wa uadilifu, dini ya kisayansi, imeuongoza kwenye "tundu la kila ndege wa kuchukiza na walio mchafu," kama Biblia ilivyosema. Na tusome jambo hilo, Ufunuo 18. Wakati tu tunapoanzisha jambo hili, tufungue Ufunuo 18:1 hadi 5. Nafikiri nimeandika hilo vizuri.

> *Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake.*
>
> *Akalia kwa sauti kuu*, (sasa enyi watu mlioota zile ndoto)... *akisema*, Unaanguka, unaanguka *Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu...ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;*

*Kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake* (kanisa)*, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake.*

*Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.*

*Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu* hukumbuka uovu wake.

46 Ni onyo la namna gani! Hilo linalitupilia kanisa kule nyuma hasa kwenye Ufunuo 3:14, kwenye wakati wa Laodikia, kuasi; wa kidini hasa, lakini ni waasi. "Wewe, kwa sababu unasema ya kwamba, 'Sisi ni matajiri, hatuna haja na kitu,' wala hujui ya kwamba wewe ni uchi, mwenye mashaka, kipofu, wala hujui." Kulingana kabisa na Maandiko ya wakati huu, si kwa Maandiko ya wakati wa Danieli, si kwa ya wale katika jina la . . . wakati wa Nuhu, lakini katika wakati huu wa mwisho, mwovu.

47 Angalieni hapa, "Wewe ni uchi." Hebu hilo likolee kabisa kabisa. Ninajua huenda nipingwe sana katika wazo hili, lakini imefikia mahali ambapo ni vigumu kwa Mkristo kutoka nyumbani mwake bila kuletwa mbele ya wakati huu mwovu, kwa njia ya wanawake waliovalia nusu.

48 Enyi wanawake, nitasema jambo hili, nami nawatakeni msikilize. Na, wanaume na wanawake, huenda msikubaliane na jambo hili, lakini ninajisikia kuongozwa kulisema. Hivi mlijua, mwanamke ye yote anayevua nguo zake namna hiyo hana akili timamu? Je! mnajua, yeye ni, aamini asiamini, ama hafikirii hivyo, yeye ni kahaba? Ingawa mwanamke huyo anaweza kusimama ameweka mkono wake mbele za Mungu na kuapa ya kwamba yeye hajaguswa na mwanamume mwingine ye yote ila mumewe, na hiyo inaweza kuwa ni kweli kabisa, bali hata hivyo yeye ni kahaba. Yesu alisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Na huyo mwanamke anaweza kuwa . . .

49 Mnaona, yeye yu "uchi," Biblia ilisema, "wala hajui." Roho anayempaka mafuta kufanya jambo hilo ni roho mwovu, wa kikahaba. Utu wake wa nje, mwili wake, nyama zake, huenda akawa msafi. Huenda yeye asifanye uzinzi wo wote, na anaweza kuapa mbele za Mungu na iwe ni kweli, ya kwamba yeye kamwe hajazini, lakini roho yake ni roho ya kikahaba. Yeye amepofushwa sana na mungu wa ulimwengu huu wa mitindo; yeye anajivalisha kizinifu akatoka kule nje.

50 Juzijuzi, mimi na Ndugu Woods tulikuwa tukiingiza mashua zetu mtoni. Nilikuwa niende mbali na nyumbani kwa dakika chache, kwenda upande wa juu wa mto. Na po pote ulipoenda, wanawake wakiwa na ninii hizi ndogo za . . . zinaitwa 'kini ama cho chote kile, wamejizungushia. Hii ni fedheha. Mwanamke

hawezi kuwa na akili zake timamu na kuvaa kitu kama hicho. Yeye amepagawa na roho ya kikahaba. Sasa, wewe tatua jambo hilo na Mungu, ewe bibi, maana utatambua siku moja ya kwamba hiyo ni Kweli.

51 Ungewezaje, bibi, ukijua jinsi mwili wako ulivyo wa heshima sana, na kuuanika kule nje kwa haya mashetani yenye tamaa mbaya na yenye dhambi yanayotembea kwenye mitaa ya siku hizi? Kama wana wa Mungu wote wangalikuwa bado ni wana wa Mungu, mumeo alikuwa mwana wa Mungu, aidha angekufanya uvae nguo ama akuache. Kama mvulana alikuwa mwana wa Mungu, asingeoa kitu kama hicho kamwe. Mnaona?

Mnasema, "Unafa-. . ." La.

Ninawaambia Kweli, na siku moja mtakutana Nayo. "Uchi, mzinzi; hujui."

52 "Loo! ninaapa ya kwamba mimi sikuvunja nadhiri za mume wangu." Mumeo atakuhukumu kwa jambo hilo kama ulizivunja. Lakini Mungu atakuhukumu kwa aina ya roho uliyo nayo ndani yako; si kukuhukumu kwa mwili wako, bali kwa roho yako, yule mtu wa ndani.

53 Mtu wa nje ni mtu wa kimwili ambaye anatawaliwa na hisi sita . . . ama hisi tano, hasa. Mtu wa ndani ni mtu wa roho ambaye anatawaliwa na hisi tano; dhamiri, na upendo na kadhalika. Mtu wa nje; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia.

Lakini ndani ya roho huyo kuna nafsi, nayo inatawaliwa na kitu kimoja, hiari yako. Unaweza kukubali anayosema ibilisi ama ukubali anayosema Mungu. Na jambo hilo litaamua ni roho wa aina gani aliye mle ndani. Kama ni Roho wa Mungu, atakula mambo ya Mungu, wala hatakula cho chote cha ulimwengu. Yesu alisema, "Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakujaingia kwenye sehemu hii ya ndani." Shetani amekudanganya. "Na mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Angalia sasa, tunaona ya kwamba yeye yu "uchi," mchafu na uchi.

54 Na ulimwengu unaonekana kuwa katika wakati ulio mwovu sana uliopata kuwepo. Wanawake kamwe hawajapata kutenda namna hiyo katika wakati wo wote, hawajatenda hivyo kamwe ila kabla tu ya kule kuangamizwa kwa ulimwengu ulioitangulia gharika. Na Yesu alirejea kwenye jambo hilo. Tutafikia jambo hilo baada ya kitambo kidogo.

55 Hivi Mungu ameshindwa kuongoza, ama Yeye anaruhusu tu mjumbe mwingine kuongoza? Sijui. Jibu la kweli la swali hili ni, kwa maoni yangu, kuna roho mbili zinazopingana ulimwenguni leo, zinazotenda kazi. Sasa, hakuwezi kuwa na zaidi ya wawili, viongozi wawili. Na mmoja wao ni Roho Mtakatifu akitenda

kazi; huyo mwingine ni roho ya ibilisi, na, katika siku hii ya mwisho, katika udanganyifu.

Sasa nitawekea msingi mawazo yangu papa hapa kwa somo lililobakia, ninii lililobakia . . . Ujumbe wetu.

56 Hizo roho mbili. Moja ya hizo, ni Roho Mtakatifu wa Mungu; huyo mwingine, ni roho ya ibilisi, ikitenda kazi katika undanganyifu. Watu wa duniani sasa wanajichagulia.

Roho Mtakatifu yuko hapa akimwita Bibi-arusi wa Kristo atoke. Yeye anafanya hivyo kwa kumthibitishia Neno Lake la ahadi Kwake, kwa ajili ya wakati huu, akionyesha ya kwamba Hilo ni Kristo.

Kama kidole kinapaswa kusogea katika wakati huu, kidole kitasogea. Kama mguu unapaswa kusogea katika wakati huu, huo mguu utasogea. Kama jicho linapaswa kuona katika wakati huu, jicho hilo litaona. Mnaona?

Roho wa Mungu, wakati anapokuwa akafikia kimo kikamilifu cha Mungu, ndio wakati tunaoishi sasa. Roho Mtakatifu yuko hapa akidhihirisha Ujumbe wa wakati huu. Naye Roho Mtakatifu anafanya jambo hili, ili kwamba watu wanaomwamini Mungu wataitwa watoke kwenye mchafuko huu.

Roho mchafu wa ibilisi yuko hapa akiliita kanisa lake kwa upotovu, kama kawaida, kwa kupotosha Neno la Mungu, kama alivyofanya hapo mwanzo.

Angalieni likirudi moja kwa moja kweye wakati ule wa mbegu tena; kutoka Edeni, hii hapa tena.

57 Sasa, kurudi kule nyuma, wewe ni wa . . . nyakati zingine, ulikuwa mfuasi wa madhehebu, ulikuwa mfuasi wa *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Ilikuwaje kwa ule ubua wa kimadhehebu? Unakauka. Roho anaendelea kuondoka na kuendelea, na inaishia kwenye Mbegu. Mnaona?

58 Na majaribio, ya wote wawili, yanarudi jinsi ile ile yalivyokuwa hapo mwanzo. Angalia. Usi-—usi, la, usisahau jambo hilo sasa.

Kama Yohana, Yohana wa Kwanza 4:5 na 6, kama ukitaka kuandika jambo hilo, yeye anasema, "roho ya upotevu."

Hawa hakuondoka tu, kirahisi, akasema, "Mimi siamini Mungu." La. Yeye aliamini kosa.

59 Shetani hakutoka na kusema, "Loo! vema, hilo hata si Neno la Mungu." Yeye alikubali Hilo lilikuwa Neno la Mungu, lakini aliweka fasiri yake mwenyewe Kwake. Ambapo, Mungu aliwaambia dhahiri wasifanye jambo hilo.

Jambo hili linafanya nini? "Linaleta nguvu za upotevu, watu wauamini uongo, na wahukumiwe nao." Sasa ukitaka kusoma jambo hilo, Wathesalonike wa Pili 2:11.

60 Kwa kuwa nina ninii, maandiko kadha hapa, na hatutaweza kuyasoma yote. Mara moja mara kwa mara, nitawapeni ninyi. Kwa kuwa linaonekana jambo la kigeni, kwamba mnaulizia jambo hilo ama kitu fulani, nasi huenda tukaliandika na kulisoma kwa manufaa ye—yenu.

61 "Kuleta nguvu za upotevu," kama Biblia ilivyosema ingefanya, Wathesalonike wa Pili. "Sasa, mtu huyu wa kuasi angetokea, na kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kwamba alikuwa Mungu, na kuwafanya watu waingie katika nguvu za upotevu, wauamini uongo; na, wauamini, watahukumiwa nao."

Hilo ndilo jambo lile lile alilomfanyia Hawa. Akampa yeye. . .Kamwe—kamwe hakumwambia Neno halikuwa kweli, bali alimpa nguvu za upotevu, hata akauamini uongo.

62 Nguvu za upotevu ni za ibilisi. "Mashetani sasa wakitenda kazi katika wana wa kuasi." Kuasi nini? Wana wa siku hizi wanaasi nini? Ni kama Hawa alivyoasi, hapo mwanzo, Neno la kweli la Mungu. Hiyo ni kweli. Sasa kama mngetaka kupata jambo hilo . . .

Na tulifungue, Waefeso 2, kwa dakika moja tu, maana inaonekana ni vizuri kwamba sisi. . .Nitasimama kwa dakika moja tu, kama hamna haraka sana, na kusoma baadhi ya haya. Waefeso 2:1 mpaka 2.

> *Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;*
>
> *Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi;*

63 "Wana wa kuasi." Na kama mpinga Kristo, akianza kule katika utoto wa kuasi, itakuwaje wakati atakapoishia katika utu wa mpinga-Kristo? Jinsi itakavyokuwa danganyifu! Ni udanganyifu wenye nguvu zaidi jinsi gani mtu—mtu mzima anaweza kuutolea ulimwengu, kuliko wa mtoto mchanga! Naye akasema, "Roho ya—ya upotevu inayotenda kazi katika wana wa kuasi," kuasi Neno. Angalia. Sasa nataka kukaa kwenye jambo hili kwa dakika moja tu, wana wa kuasi," mwana.

64 Hivi ulijua, wewe, mwanzo wako, ninaweza kuthibitisha kwa Neno la Mungu ya kwamba wewe, mtu ye yote aliye humu ndani, ulikuwa hai katika babu wa baba yako. Na babu wa baba yako, ulizaliwa kupitia kwa babu, halafu baba yako, halafu wewe. Unajua jambo hilo?

Biblia ilisema, ninaamini ni Waebrania 7, ya kwamba, Melkizedeki, Ibrahimu aliporudi kutoka kuwapiga wafalme, "Ibrahimu alimpa Melkizedeki sehemu ya kumi ya nyara zote." Na huyu hapa Paulo akisema sasa, ya kwamba, "Lawi,

aliyepokea sehemu ya kumi, alikuwa bado . . . Yeye alitoa sehemu ya kumi, kwa kuwa alikuwa yuko bado katika viuno vya Ibrahimu hapo alipokutana na Melkizedeki." Kwa hiyo lo lote alilofanya Ibrahimu, ndipo tunaona ya kwamba Lawi alikuwa katika Ibrahimu wakati huo, ambaye alikuwa mzaa babu yake. Ibrahimu akamzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo akawazaa wazee wetu, Lawi.

Sasa, basi, unaona, hapa kunaonekana wazi, kuchaguliwa tangu zamani.

65 Sasa, katika Jumbe hizi, ninataka ku—ku—kutilia mkazo mambo niliyowaambia katika Ujumbe, wa Nuru hii ya jioni ambayo Mungu alisema ingekuja duniani.

66 Pia angalieni, basi, "Mnyama aliyekuwa aje duniani, angewadanganya wote ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia."

67 Katika mawazo ya Mungu mwenyewe; Mungu, yule Roho mkuu. Hapo mwanzo, kabla hapajakuwepo na mwanzo, Yeye alikuwa ni Mungu, na hivi ulijua ulikuwa ndani Yake wakati huo? Kama wewe ni Mkristo sasa, ulikuwa ndani yake wakati huo.

Na halafu, kama hivyo ndivyo ilivyo, ukamilifu wote wa Mungu katika mwili uliumbika katika Utu wa Yesu Kristo. Ndipo wakati Yesu alipokufa msalabani, nilikufa pamoja Naye, kwa maana nilikuwa ndani Yake wakati huo; kwa maana Yeye alikuwa utilimilifu wa Neno, lililodhihirishwa, akijua ya kwamba sisi tungedhihirishwa baadaye. Nasi tulikuwa pale Kalvari pamoja Naye. Tuliingia kaburini pamoja Naye. Nasi tulifufuka pamoja Naye na kufufuka Kwake. Na sasa tumepanda, kwa Roho Wake, kwenye Kiti cha Enzi cha neema, tukiketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. Daima!

68 Kwa kuwa kama vile chembechembe ya maisha ya kawaida ilivyoshushwa, ikapata uhai kutoka kwa baba, kuingia kwa kwa baba, kuingia kwa baba, kuingia kwa baba, vivyo hivyo ndivyo Uzima wa Kristo ulivyo hai.

Hiyo ndiyo sababu ya Mungu hutumia Roho ya Eliya mara tano mbalimbali. Ni kitu gani? Ni kupokezana.

69 Ni kama tu vile uhai wako wa kawaida na tabia inavyoridhiwa na kuzaliwa kwa asili kwa baba yako, ndivyo alivyo Roho wa Mungu, aliyechaguliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Na wakati Neno lote la Mungu, katika ukamilifu, lilivyokuwa katika mwili wa mwanadamu ulioitwa Yesu Kristo, mle ndani Mungu alinifanya kulipia dhambi zangu, katika Yeye pale. Ndipo akanifufua, akanifufua pamoja Naye, katika ufufuo.

Na sasa tumeketi pamoja Naye, tukiwa na nguvu na mamlaka juu ya kila pepo. Loo! laiti ungaliamini tu kile Mungu ametoa! Bali kama wewe hujaketi pale, huna kitu hicho. Na iwapo umeketi pale, na huamini, ama unaogopa kusogea, hutaitumia kamwe. Lakini kama umeketi pale, utaitumia, kwa maana umechaguliwa kufanya yale unayofanya.

70 "Farao," ule upande mwingine, "aliinuliwa awe Farao kwa kusudi hili," Biblia ilisema. "Yuda Iskariote aliinuliwa kuwa mwana wa upotevu."

Sasa angalia Kweli hizi kuu ambazo tunazikaribia.

71 Sasa tunaona ya kwamba kanisa lilikataa kukubali Neno la Mungu liwatawale, na likamkubali Baraba badala yake. Sasa, kama unataka Maandiko juu ya jambo hilo, ni Mathayo 27:15 mpaka 23. Hili lilifanya nini? Hili lilifanya kazi mahali gani? Sasa wazia jambo hilo. Wakati kanisa la ulimwengu, katika maisha yake ya utaratibu wa mtu mwenye haki, mtakatifu, kama walivyodhani walikuwa, na walikuwa hivyo katika macho ya watu, wao walimsulubisha Yesu, na kusema, "Hatutaki Mtu huyu atutawale." Naye Yesu alikuwa utimilifu wa Neno la Mungu. Yohana wa Kwanza 1, inaeleza jambo hilo. Nao walisema, "Hatutaki Neno hili la Mungu litutawale." Hata hivyo, Yeye alikuwa ni Neno, bali macho yao yalipofushwa wasijue Yeye alikuwa nani. Kwa kuwa Yeye alikuwa jawabu la moja kwa moja kwa kila unabii uliokuwa utimie ndani Yake.

Sasa, sote tunaamini jambo hilo, kwa sababu tunaangalia nyuma kuona hayo yakitukia. Lakini kama ulimwengu ungeweza, huu uliopo sasa, wakati huu mwovu wa sasa, ambao ungalikuwa kule nyuma wakati ule, wao wangefanya jambo lile lile wanalofanya leo, kwa sababu lingali ni Neno lile lile, kwa ajili ya wakati huu, likidhihirishwa. Wao watafanya jambo hilo. Hawawezi kufanya jambo lingine. "Wao ni wana wa kuasi." "Wamepewa nguvu za upotovu, kuamini uongo, na wahukumiwe nao."

72 Angalieni wakati ulimwengu wa kanisa usingemkubali Yesu, Neno, lililodhihirishwa la siku ile, kwa sababu (kwa nini?) walikuwa wamelifasiri kwa njia nyingine. Lakini walipaswa kujua ya kwamba Yeye alikuwa hilo Neno, kwa sababu kila kitu ambacho Mungu alisema angekifanya, Yeye alikifanya. Naye aliwaambia, "Yachunguzeni Maandiko ya wakati huu; na kama Mimi sitimizi masharti yaliyonenwa nitayatimiza, basi msiniamini Mimi."

Wakasema, "Tunamwamini Musa."

73 Akasema, "Kama mngalimwamini Musa, mangaliniamini Mimi, kwa maana Musa alinena habari zangu Mimi." Na hata hivyo hawakuona jambo hilo. Mungu yule yule wa Mbinguni akifa msalabani, na akitamka maneno yale yale nabii aliyosema

Yeye angeyasema, na hata hivyo wao hawakuona jambo hilo. Mnaona?

Wao hawakuwa wa aina Yake. Hawakuwa Neno, hawakuwa Neno; nao, hata hivyo, walikuwa—walikuwa wa dini sana. Bali hawakuwa Neno, kwa maana Hilo—Hilo lingetambua mahali Pake kwa ajili ya wakati huo.

74 Angalia jinsi Maandiko yanavyojifunganisha vizuri katika kila wakati. Angalia sasa.

Na wakati ulimwengu wa kanisa haukutaka Neno la Mungu liwatawale, wao walimkubali mwuaji, Baraba. Hili lilifanya jambo gani? Lilimkuza Shetani, mungu wa wakati huu mwovu, kufikia mahali ambao alipataka daima.

Sasa sikilizeni. Kwa kuwa, Shetani hanenwi kama mungu wa wakati mwingine wo wote ila huu. Hakunenwa kama mungu wa wakati wa Nuhu. Hakunenwa kama—kama mungu wa wakati wa Musa, mungu wa wakati wa Eliya. Lakini, wakati huu mwovu, yeye ni . . . Loo, msikose jambo hilo! Yeye ni mungu wa wakati huu mwovu, akiabudiwa na mamilioni na mabilioni ya watu, nao hawajui jambo hilo. Lakini hebu tuachilie Maandiko yamfunue asubuhi ya leo, na hebu tuone, ndipo mtajua. Hebu Maandiko . . .

75 Kama vile katika mikutano ya upambanuzi, wakati Roho Mtakatifu anapoingia katikati ya Neno Lake Naye anamwita mtu huyu na kusema, "Huna shughuli ya kuishi na mwanamke huyu mwingine. Kwa nini ukafanya jambo hilo, miaka kumi iliyopita, wakati ulipomtorosha mke wa mtu yule?" Yeye anafanya nini? Unamfunua, anamfunua Shetani wazi, ambaye amemfunga mtu huyo, ama mwanamke anayeishi na mume wa mwanamke mwingine, ama dhambi ambazo wamefanya, mambo ambayo wamefanya. Linafanya nini? Linamfunua.

76 Madaktari wanachukua vyombo na kujaribu kuona kuna nini. Hawawezi kufanya hivyo. Hatujui. Lakini basi Roho Mtakatifu anakuja na kufunua yeye ni nini, na kumfunua wazi. Mnaona? Hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo. Ni nuru inayowaka gizani.

Na wakati unapochukua kelele fulani chumbani, inasikika ya kisiri-siri; dude linapiga makelele, wala hujui ni nini. Washa taa, upesi . . . Nyenje, kombamwiko, wao—wao ni wana wa gizani. Na wakati nuru inapomulika, wao hutoroka.

"Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wetu," Biblia ilisema. Mnaona? Wao hawawezi kuishi katika Nuru ya ulimwengu . . . Kwa kuwa, Mungu wa Mbinguni ametuma Nuru Yake katika siku hizi za mwisho, ili kwamba aweze kuwaangazia watoto Wake njia, wasije wakatembea gizani na kujikwaa, bali wapate kutembea katika Nuru ya kunawiri kwa Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina!

77 Angalia, Shetani haitwi mungu wa wakati mwingine wo wote bali huu. Tamaa yake ilikuwa ni kuwa kama Mungu, tangu mwanzo kabisa.

Hebu tusome jambo hilo. Tutachukua tu wakati wetu. Hebu turudi nyuma kwenye. . . Mnaona, nimeiandika hapa, Isaya 14. Hebu turudi nyuma hapa kwenye Isaya 14, kwa muda kidogo tu, tuone yale aliyosema Mungu. "Mungu," aliyofanya Shetani. Isaya 14:12 na 14. Angalia.

> *Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, ewe uliyewaangusha mataifa!*
>
> *Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu;* (wana wa Mungu, sasa) *nami nitaketi* pia *juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kaskazini.*

78 Tamaa ya Shetani ilikuwa ni kuabudiwa kama Mungu. Alichukua theluthi mbili, theluthi mbili za nyota za Mbinguni. Akapanda juu ya nyota hizo, na kuwahubiri, na kuwadanganya theluthi mbili. Mnaona jambo hilo? Vema. Angalieni, hiyo ndiyo tamaa yake.

Na sasa yuko tayari, kwa bibi-arusi wake aliyechaguliwa kwa uangalifu, akasomeshwa kwa maarifa yake, mnaona, anajipodoa na udanganyifu, wa majumba makubwa makubwa na madhehebu makubwa, na rangi za maarifa na theolojia, na ni mwerevu na mwenye bongo nyingi, na amesoma, apate kuudanganya ulimwengu mzima, na kuwa "mungu." Hivyo ndivyo amefanya. Yote yanaelekea kwenye utu wa mpinga-Kristo, ambaye tayari amewekwa taji "halifa wa Mungu," na bibi-arusi wake wa kisayansi anayeyapenda ya ulimwengu, amevalishwa katika fahari ya elimu ya kiakili na ya kidini. Amefanywa wa kidini kama yeye, na kwa fasiri yake mwenyewe ya Neno la Mungu kama alivyomfanya Hawa, na kama allivyofanya mwanawe, Kaini.

Sasa mlisema, "Ati mwana wa Shetani?"

79 Nionyeshe mahali pamoja katika Biblia ambapo Kaini alipata kuitwa mwana wa Adamu. Biblia ilisema alikuwa "mwana wa yule mwovu," uzao wa nyoka. La, kifuniko kimeondolewa sasa, ndugu. Piramidi imefunguliwa, kama vile ufunuo ulivyoonyesha.

80 Angalia yale atakayofanya, mawazo yake. Yeye alifikiri Mungu aliishi katika urembo wa kiulimwengu. Yeye alifanya jambo hilo Mbinguni. Dhambi haikuanza kamwe katika bustani ya Edeni; ilianza Mbinguni, wakati Lusifa, mwana wa asubuhi, alipojiinua katika uzuri, na kutaka ufalme unaopendeza zaidi kuliko ule wa Mikaeli. Naye alidhani ya kwamba Mungu aliishi katika uzuri.

81 Basi angalia Kaini. Yeye hakutaka dhabihu ya damu. Yeye alishuka akatoa sadaka ya tunda, ama—ama mashamba ya uzuri kwenye madhabahu yake. Wa dini sana, alifanya kila kitu, kile, vile vile kabisa alichofanya Habili; akatoa dhabihu, akapiga magoti mbele za Mungu katika ibada, mtiifu kwa kila njia, lakini bila ufunuo wa Neno.

Nalo Neno lilikuwa, tangu mwanzo, mpango wa Mungu. Lakini Mungu akafunua, kwa ufunuo, jambo lile lile ambalo alithibitisha na kuhakikisha kwamba ilikuwa ni kweli. Si dini, si madhabahu, si kuwa mfuasi wa kanisa, si kutoa dhabihu, si kuwa mwaminifu; bali kwa ufunuo wa Neno la Mungu. Mungu akimfunulia kile ambacho . . .

Mama yake hakula tofaa alilopewa na nyoka, lakini alifanya uzinzi na utu wa Shetani, katika umbo la mnyama; si mnyama atambaaye, bali aliye mwerevu sana, mjanja sana kuliko wote walio kondeni, sura ya mtu, kitu pekee ambacho mbegu yake ingechanganyikana nacho. Sasa sayansi inajaribu kumpata huyo. Wala hawatampata, kwa sababu kila mfupa mwilini mwake umebadilishwa. Lakini Biblia inatangaza kwamba jambo hilo ni kweli.

82 Angalia yale jamaa huyu atakalofanya sasa. Jamaa huyu, "Ataketi kwenye hekalu la Mungu," hiyo ni kusema, kanisa, "akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." Sasa kama mnataka kusoma jambo hilo, hiyo ni Wathesalonike 2:3 na 4, na Ufunuo 13:4, 11 na 12; ambapo walinena, manabii wote wawili, Yohana na Paulo pia, juu ya kile atakachokuwa katika siku za mwisho. Sasa ninyi someni hilo, kwa maana nimeliandika hapa. Lakini mimi . . . kuokoa wakati sasa.

83 Siku tunayoishi inaitwa, katika Biblia, "siku ya mwanadamu," siku ya mwanadamu. Hii si siku ya Mungu. Mungu si mungu wa dunia hii; Biblia inasema siye. Yeye ni Mungu wa Mbinguni. Bali hii si siku ya Mungu.

Hii ni siku ya kujichagulia. Aidha, uishi kwa ajili ya siku hii, kisha ufe; mchague Mungu, upate kuishi. Naye Mungu ni Neno, nalo Neno ni Neno lililodhihirishwa kwa ajili ya wakati huu na siku hii.

84 Angalia, "siku ya mwanadamu." Kama ukitaka kuandika jambo hilo, nilikuwa nikitaka kulisoma. Lakini Wakorintho wa Kwanza 5:1-5 . . . Wakorintho wa Kwanza 4:1-5, samahani, Wakorintho wa Kwanza 4:1 na 5, ilikuwa ni Paulo akinena juu ya kuhukumiwa na mwanadamu, katika siku ya mwanadamu.

85 "Ile siku, kwa nini unaiita siku ya mwanadamu?" ungesema. Ni siku ambayo kazi za maarifa ya mwanadamu zinatukuzwa.

Angalia ambapo, majivuno yote ya wakomunisti, mtu fulani akijaribu kumpeleka binadamu mwezini. Mungu anajaribu kupeleka mtu fulani Mbinguni. Mnaona? Lakini angalia jinsi wanavyotumia mamilioni na mabilioni na matrilioni ya dola,

katika jitihada za bure. Watakapofika kule, hawatapata kitu. Imekuwaje kwao?

Sijali kuhusu mwezi. Ninataka kupita mwezi upesi sana hata sitauona; nitaendelea tu kupanda juu zaidi. Ninataka kupita lile Kundi Jeupe la Nyota, niendelee, nizidi kwenda tu. Naam!

86 Na ulimwengu leo unajitolea kwa maarifa ambayo yanatokana na Shetani. Nayo siku ya mwanadamu inatukuzwa, si na Neno la Mungu, bali na maarifa aliyo nayo.

Sasa wazia. Hebu hilo likolee. Na utakapocheza kanda hii, ufikapo mahali hapa, ifunge muda kidogo uwazie.

Kazi zake zinakuzwa zaidi ya Neno la Mungu na kazi zilizodhihirishwa; hekima ya Shetani, aliyompa Hawa hapo mwanzo. Sasa sikilizeni; msikose jambo hili. Hekima ya Shetani imeinuliwa kwenye kiti cha enzi cha kuabudia, katika mwanadamu, juu ya Neno lililothibitishwa la Mungu la wakati huu. Makanisa yetu yanathibitisha jambo hilo kwa ninii zao—seminari zao, shule za kusomea, ambazo mnasoma zaidi ya Neno la Mungu linavyojua habari Zake, ndivyo wanavyodhania. Na kule, Daktari *Fulani*, na Mwalimu *Fulani*, na Profesa *Fulani* wameinua maarifa yao wenyewe, yanayodhaniwa (kutoka kwa Shetani) kwamba ni kweli, juu ya ahadi ya Mungu iliyothibitishwa, ikadhihirishwa moja kwa moja mbele zao. Naye mwanadamu anaikubali vizuri kabisa. Mnaona?

87 Mafanikio yake ya kisayansi, akijaribu kuthibitisha Neno la Mungu kwamba ni uongo. Wazia tu jambo hilo. Yeye, yake, hiyo ni kusema, theolojia ya mwanadamu, huwafafanulia watu Neno la Mungu, na kulifanya lisiwe na nguvu kwa watu tena, kama alivyofanya katika wakati wa kimadhehebu wakati Yesu alipotokea duniani. Yesu alisema, "Enyi wanafiki! Ninyi, kwa mapokeo yenu," hayo ni tafsiri yao, "mmechukua Neno la Mungu na kulifanya lisiwe na nguvu kwa watu." Na hilo ni jambo lile lile walilofanya leo. Halina nguvu.

88 Angalia, "Wao," hao watu, "wanamwinua juu ya yote yaitwayo Mungu." Je! Wathesalonike wa Pili haisemi wao wangefanya jambo hilo? Na mamlaka ya kanisa la kimadhehebu, watu wakiyaamini hayo madhehebu zaidi kuliko wanavyomwamini Mungu. Naye Mungu ni Neno. Wao wataamini kanuni zao za kimadhehebu kuliko Neno, ambao "wanamwinua juu ya kila kiitwacho Mungu." Na kuna Mungu mmoja tu, na huyo ni Neno.

"Yote yaitwayo Mungu; hata yeye kama Mungu huketi katika hekalu la Mungu, akithibitisha ya kwamba yeye ni Mungu," kwa sababu amewafanya watu wamwabudu. Mungu ni Neno. Naye anajiinua juu ya kila kiitwacho Mungu. Na kuna Mungu mmoja tu, na Mungu huyo ni Neno. Mnaona? "Na yote yaitwayo Mungu," ni kwamba, mungu wa wakati huu amejiinua mwenyewe juu ya Neno la kweli la Mungu lililothibitishwa. Hiyo

ni Yohana Mtakatifu 1. Mnaona? "Juu ya yote yaitwayo Mungu, hata yeye kama Mungu huketi katika hekalu ya Mungu," akiwa na mamlaka.

Angalia, na yeye anasifiwa kwa jambo hilo! Loo! wajalie watu, Mungu, waone udanganyifu huo! Yeye anasifiwa kwa jambo hilo, na kuaminiwa kwa uchaji na watu wa wakati huu mwovu. Sasa mnaona mungu na watumishi wake wa wakati huu mwovu?

89 Sasa hebu tuangalie likidhihirishwa. Yeye anasema anatengeneza ulimwengu mzuri zaidi kuishi humo, kwa maarifa yake mbali na Neno la Mungu lisiloshindwa. Lakini kwa kukusanyika kwake, katika madhehebu, na kanuni za imani, na akili, na kisayansi, na kadhalika, yeye anatengeneza ulimwengu bora zaidi wa kuishi mwanadamu, akipuuza ahadi ya Mungu, ya kwamba wakati tu ambapo ulimwengu utafaa kwa kuishi ni katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Mwajua, maoni yangu, yeye ametengeneza ulimwengu bora zaidi kwa kufanyia dhambi badala ya wa kuishi humo.

90 Angalia. Yeye alifanya jambo hilo? Alihalalisha dhambi. Alihalalisha kunywa wiski, kuvuta sigara. Na katika makanisa, alihalalisha ya kwamba mwanamke angeweza kuwa mfuasi wa kanisa, akiwa na nywele fupi. Sasa hebu tulieni kwa muda kidogo.

91 Yeye anaweza kuvaa suruali fupi, kujipaka vipodozi, na bado awe ni mfuasi wa kundi lake la dini, jambo ambalo ni kinyume kabisa na Neno la Mungu. Yeye anasema ni sawa. Mnaona maarifa yake? "Hilo lina uhusiano gani na mwanamke?" Ni kama tu kule kula tunda lililokatazwa, ama kutokula tunda lililokatazwa, hivyo ndivyo ilivyo. Mungu alimwambia asifanye hivyo, bali yeye anafanya hivyo.

92 Naye anamwamini, na anampenda kwa ajili ya jambo hilo. Yeye anamchukia Mungu. Matendo yake mwenyewe yanathibitisha ya kwamba anamchukia. Yeye anasema anampenda, bali anampenda Shetani. Anamwabudu mungu wa mtindo, mungu wa dunia, mungu mke wa Hollywood. Anampenda, lakini analichukia Neno la kweli la Mungu, ambaye ndiye Mungu wa kweli aliyepo.

Alilihalalisha makanisani. "Hakuna madhara. Wanawake wetu wanaweza kufanya jambo *hili*, *lile*, ama *lingine*. Lakini katika Uwepo wa Mungu aliye hai, hata haruhusiwi kuja, isipokuwa anatubu.

93 Anaona, yeye ni mungu wa ulimwengu wa urembo, ndivyo alivyo. Anataka kuonekana mrembo. Naye ni mungu wa urembo, tangu mwanzo. Anaweza, na amefaulu kwa maarifa yake katika sayansi na vitu mbalimbali, kutengeneza urembo kwa ninii yake, wakati huu wa mitindo . . . wakati huu wa kisasa, hasa, mwovu. Umefanywa mrembo.

94 Angalia. Ni jambo muhimu kuangalia. Hapo mwanzo, Sethi na watoto wake hawakupitia njia ya kisayansi.

Sasa tutazungumza juu ya sayansi kwa dakika chache. Kama nikisema jambo hili, si kutoa udhuru kwa ajili ya ujinga wangu; lakini, kundi la wapumbavu, kitu cho chote kitakachokana Neno la Mungu. Mnaona? Hakika.

Inastahili kuangaliwa. Angalia jambo hilo. Watoto wa Sethi hawakuiendea njia ya kisayansi. Wao walikuwa wachungaji wanyenyekevu, wakulima, na kadhalika.

Lakini wana wa Kaini waliiendea. Kwa nini? Walitiwa upako na baba yao, ibilisi. Kaini, alitiwa upako na babaye, ibilisi, na hawa walitiwa upako na hiyo mbegu ikipokezanwa.

95 Angalia mbegu ya Mungu ikija katika kila wakati, na uangalie mahali inapoelekea leo. Wakristo, Wakristo halisi, hawashughuliki sana na utafiti wa sayansi na kadhalika. La. Hebu kidogo, tutaingilia jambo hilo.

Lakini wa Kaini walifanya hivyo, kufuatana na tabia ya baba yao, ibilisi, aliyejaa maarifa ya kilimwengu, urembo, na sayansi, na kadhalika. Watoto wa Kaini walikuwa wa kisayansi. Walikuwa na elimu. Walikuwa wachezaji wa muziki—vifaa vya muziki; Elvis Presley wa kisasa, baadhi ya upuzi kama huo ambao halmashauri ya shule inaruhusu utendeke hapa kwenye kichochoro hiki kila Jumamosi usiku. Wajenzi wa mji, wakiwapodoa wanawake kwa ajili ya tamaa za kibinafsi, kama vile ibilisi anavyowapa wanawake vipodozi, na kukata nywele zao, na kuwavalisha kaptura, na mambo kama hayo. Wao, ni kwa ajili ya tamaa zake chafu. Hilo ni kali sana, lakini sijui njia nyingine yo yote ya kulisema.

96 Sasa, tunajua injili ya Shetani ni injili ya sayansi na ufanisi. Yeye aliihubiri huko Edeni; si Mungu; Shetani aliihubiri, sayansi ya ufanisi. Sayansi na ufanisi ndiyo injili ya Shetani. Angalia mahali ambapo ametuelekeza leo, nayo. Mnaona?

97 Angalia, yeye aliihubiri huko Edeni, kwa nani? Kwa bibi-arusi wa Adamu. Naye akashawishika vizuri sana. Alimdanganya mpaka akahoji moja ya Maneno ya Mungu. Hebu tuone jambo lile huenda yeye alilisema. Hapana budi alisema, "Si jambo la kisayansi kufa, katika kanisa hili takatifu." Ama, "Utafundishwa na kuelimishwa, kutokumini kitu cha kijinga hivi kama mauti. Sijali kama Neno la Mungu lilisema jambo hilo; ni la kijinga."

98 Loo! mwangalie leo. "Mungu ni Mungu mwema. Uko katika kanisa Lake takatifu; mbona, huwezi kufa." Lakini Mungu alisema ungekufa, na hilo latosha. Unamwona leo? "Loo! kuwa tu mfuasi wa kanisa. Si yale ufanyayo, ama *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Njoo tu kanisani na uwe mshiriki mzuri. Kukata nywele zako, huo ni upuzi. Na kuvaa kaptura, kujipodoa, na kwenda kwenye madansi, na pombe kidogo mara moja

moja, haitakudhuru, mradi tu huizoelei. Kwa kweli, laiti ninyi watoto mngaliinywa, ili kwamba wajue kama wangeipenda ama wasingeipenda." Huyo hapo, mungu wa wakati huu, wakati huu mwovu.

99 "Mungu ni Mungu mzuri." Nimesikia jambo hilo sana hata linanichefua. Mungu ni Mungu wa haki pia. Yeye si babu mkongwe aliyepungukiwa na akili na nguvu, ambaye anaweza kusukumwa-sukumwa, na wajukuu wake hawana dhambi yo yote. Yeye ni Mungu mwenye haki na utakatifu. Alithibitisha jambo hilo katika bustani ya Edeni, kwa watoto Wake wa kwanza. Ukivuka mstari huo, wa moja ya Maneno Yake, umekufa. Ni jambo lile lile leo.

100 Angalia pia, yeye alimhubiri Hawa injili ya namna hiyo ya kisayansi, ya jamii, ya kielimu na maendeleo, naye bibi-arusi wa Adamu akaiamini. Naye amefanikiwa katika kumjaza anayejiita bibi-arusi wa Kristo, kanisa la Adamu wa Pili, kwa hoja zile zile. Hiyo ni kweli.

101 "Loo, si—si kwa Mungu; Mungu ni mzuri sana hawezi kufanya jambo hilo. Mbona, mradi tu unahudhuria kanisa. 'Kama unaamini.'" Ibilisi anaamini; si kujifanya anaamini, bali anaamini kweli. Hajaokoka. "'Kama unaamini.'" A-ha!

102 Yeye anamwambi bibi-arusi wa pili, ama Bibi-arusi wa Adamu wa Pili, vile vile alivyomwambia yule wa kwanza. Kitu kama, "Naam, kuponya Kiungu, hakuna kitu kama hicho. Tunaweza kuthibitisha jambo hilo. Hakuna kisa kilichowahi kuthibitishwa." "Na ubatizo huu katika Jina la Yesu, sasa hivi hutambui ya kwamba mimi ndimi mamlaka ya kanisa?" yeye anasema. "Tumemaliza jambo hilo huko Nikea, Rumi," wakati zile roho tatu chafu zilipotoka kwenye yule joka, manabii wa uongo, na kadhalika. "Tunaamini kuna utatu wa Miungu." Loo, jamani! Huo ni upagani kwelikweli. Usimkaribie Mungu kamwe ukiwa na kitu kama hicho, kujaribu kusimama katika Uwepo Wake. "Loo, haileti tofauti yo yote kama umebatizwa katika vyeo vya 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Inaleta tofauti gani?"

103 Ilileta tofauti kubwa sana, hata Paulo akaamuru kundi la Wabatisti ya kwamba wanapaswa kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo kabla Roho Mtakatifu hajawajilia. Na pia ilimfanya yule mtume kulia kwa sauti kuu, na kusema, "Kama malaika akitoka Mbinguni na kuhubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe." Hakika, inaleta tofauti. Loo, jamani!

104 "Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu siku hizi. Huo ulikuwa tu kwa ajili ya mitume. Umepita. Na kitu kama manabii? Hata hakijulikani. Ati miujiza? Hiyo si ya kisayansi. Malaki 4? Hiyo ilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine. Yohana 14:12? Loo! Yesu kweli hakumaanisha jambo hilo. Luka 17:30? Loo! hiyo ilikuwa tu ni hadithi ya uongo. Mnaona, li—

limefasiriwa vibaya; halikuwa katika ile fasiri ya asili." Upuuzi kama huo!

Ambapo Mungu Mwenyezi anashuka chini kati yetu na kuthibitisha jambo hilo. Wakati anaposema, ya kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," Yeye huthibitisha jambo hilo kwamba ni kweli. Sijali ni nani anayekanusha jambo hilo; Mungu hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Alisema angefanya jambo hili katika siku za mwisho. "Kutakuwa Nuru wakati wa jioni." Na kuna Nuru, kwa ajili ya kudhihirishwa kwa Mwana wa Mungu.

105 Jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linalotua magharibi. Nabii alisema, "Kutakuweko na siku ambayo haingeitwa mchana wala usiku." Ni siku yenye utusitusi, yenye mawingu, kama juu ya jua. Lakini akasema, "Yapata wakati wa jioni Nuru itakuja tena." Mwana yule yule! Ndiye Alfa na Omega. Jua lile lile lililochomoza mashariki lilibashiriwa kuchomoza magharibi tena, katika siku za mwisho, kabla tu ya siku kuisha. Sijui jinsi wanavyofasiri jambo Hilo; Mungu hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Yeye hulithibitisha Hilo. Huu ndio wakati wa jioni.

106 Ni huzuni, lakini yeye kweli alishawishika katika jambo hilo tena. Bibi-arusi wa Kristo alishawishika, na kuchukua maarifa ya kiakili ya mhubiri fulani wa seminari badala ya kuliamini Neno la Mungu lililo safi na lililothibitishwa.

107 Sasa wahudumu walio huko nje nchini po pote mlipo, huenda msikubaliane na jambo Hili. Mimi siwaudhi. Ninajari-. . . Mimi ninazungumza na kundi langu mwenyewe. Ninajaribu tu . . . Kama mnataka kuketi ndani, hakika ningefurahia ninyi mkilisikia jambo Hilo. Na ndipo mlisikilize. Mnona? Bali ninawaambia tu yale ambayo wame-—yale ambayo wameona, na kuwaonyesha jambo hilo; Mungu akilithibitisha, ya kwamba ni kweli. Mnaona?

Hii ndiyo ile saa. Halihitaji mtu ye yote kulifasiri. Maarifa yako ya kilimwengu hayana cho chote . . . Huenda ukawa na B.A. D.D., A.D., ama yo yote ile; haimaanishi hata jambo moja. Mungu hufasiri Neno Lake, Mwenyewe. Yeye aliahidi jambo hilo, na ndio hili hapa.

108 Lakini kwa maarifa ya seminari, mahubiri ya kimadhehebu, "yameifanya dunia yote imstaajabie mnyama ambaye jeraha lake la mauti lilipona," kutoka upagani kuingia ya kipapa. Mnaona mahali linakoelekea? Yeye anaamini jambo hilo. Anaamini maarifa anayomwambia.

109 Ni kwamba, sasa angalieni, ni kwamba bibi-arusi wote wawili walioposwa waliamini maarifa ya Shetani dhidi ya Neno la Mungu. Bibi-arusi wa Adamu aliamini maarifa ya Shetani dhidi ya Neno la Mungu, naye bibi-arusi wa Kristo ameamini

maarifa ya Shetani, katika wakati huu mwovu wa kiakili, dhidi ya Neno la Mungu.

Pia angalia. Hawa, katika hali ya kawaida, aliliamini jambo hilo, na kutumbukiza jamii yote ya kibinadamu mautini. Bibi-arusi wa kawaida! Adamu, mtu wa kawaida wa dunia; bibi-arusi wake, kabla hajashiriki naye, kuwa mkewe, alitumbukiza jamii yote ya kibinadamu mautini. Kama ni la kisayansi ama sivyo, tunakufa vile vile, maana Mungu alisema tungekufa.

Au uko kwenye Edeni takatifu, ama kanisa takatifu, ama madhehebu matakatifu, ama lingekuwa cho chote kile, utakufa siku utakayokosa kuamini Neno la Mungu kuwa ni Kweli, wakati limethibitishwa na kuhakikishwa kwako. Hiyo ndiyo siku unapojitenga mwenyewe na Mungu. Si sentensi nzima tu; Neno moja. "Kila atakayeongeza neno moja, ama kutoa Moja," hiyo ndiyo siku utakayokufa.

110 Angalia, Bibi-arusi wa Adamu alisababisha mauti ya kawaida kwa jamii yake, jamii ya binadamu.

Naye bibi-arusi wa Adamu wa Pili, bibi-arusi aliyeposwa kwa Kristo, ametumbukiza kanisa lote kwenye mauti ya kimadhehebu, kuchukua alama ya mnyama, kwa madhehebu makubwa ya kisayansi na kiakili. "Sisi ni Wabatisti. Sisi ni Wapresbiteri. Sisi ni Wapentekoste," na kadhalika. "Tuna *hiki*, na tuna mali nyingi zaidi. Sisi, tunajulikana na serikali. Tuko kila mahali ulimwenguni," na mambo yote kama hayo. "Na walio bora sana kuliko wote, na meya wa jiji, na kadhalika, anakuja kwetu. Hata raisi huja kushiriki misa pamoja nasi, na tunakuja kwenye *hili*, *lile*, ama *lingine*." Ulimwengu mzima umetumbukizwa katika mauti ya kiroho na ya kimadhehebu; kanisa lote. Limekufa!

Unasema, "Unachanganya mambo mengi sana."

111 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu." "Katika siku za Lutu, ambapo watatu walitolewa Sodoma, kwenye siku hiyo . . . " Sasa tayari kuna kundi limetoka, kumbukeni. "Lakini kama ilivyokuwa wakati huo, wakati Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa." Angalia ni siku ya namna gani, angalia mahali tunapoishi!

112 Sasa ameufanya ulimwengu mzima kukubali uongozi wa kisayansi wa mipango ya elimu ambayo Shetani amempa chini ya jina la kanisa, uongozi wa miradi ya kielimu na ya kisayansi. Mimi ninawaonyesha mungu wa ulimwengu huu.

Wakati yeye, kama Hawa, alipokuwa na kujazwa kabisa kwa Neno la Mungu mkononi mwake, yeye angaliweza kuchukua Neno la Mungu. Lakini yeye alifanya nini kwa jambo Hilo? Badala ya kungojea ubatizo wa Roho Mtakatifu, aliacha sayansi imthibitishie ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa kwa ajili ya wanafunzi tu.

Badala ya kuendeleza kuponya Kiungu, wakati sasa anapaswa kuwa akiwafufua wafu na kutenda miujiza mikubwa; amemwacha Shetani, chini ya uongozi wake wa mtu wa dini, achukue Neno la Mungu na kujaribu kusema ya kwamba Hilo lilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine. Naye ameamini jambo hilo.

113 Wakati, Biblia ilisema, "Mambo niyatendayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya." Yesu alisema jambo hilo. "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Sisi tungali tu viumbe. "Ishara hivi zitafuatana na kila mmoja wa hao waaminio." Yeye anakana kila sehemu Yake.

114 Anakana mambo yote ya miujiza, na aliyabadilishana na wazo la kiakili la Biblia; ambapo makasisi, na baba mtakatifu, anavyojiita, ambapo maaskofu, maaskofu wakuu, ambapo wazee wa jimbo, viongozi wakuu, na kadhalika, wameweka fasiri yao wenyewe Kwake. Naye Mungu amewaacha, waketi pale, wamekufa kama usiku wa manane.

Na jambo pekee lililobaki katika siku za mwisho ni maskini kundi la Wapentekoste wenye vifaa vya muziki wanazocheza kwa fujo, wakikimbia huku na huku sakafuni, wakinena kwa lugha na kupaza sauti, "wenye mfano wa uungu, bali wakikana Neno lake." Waambie wabatizwe katika Jina la Yesu Kristo; watakucheka waziwazi. Lakini, hapo, Mungu anaenda moja kwa moja akilifanya kuwa vile vile, akithibitisha Neno Lake kwamba ni kweli.

115 Angalia, ule mti ambao Shetani alimfanya Hawa aule, ulikuwa "mti wa mema na mabaya." Ulikuwa ni mti uliochanganyikana.

Sasa angalia siku tunayoishi, wakati Yeye anaita Bibi-arusi. Yeye ana kanisa ambalo linadai kwamba linatenda mema, wakati linatenda maovu, kwa kulikana Neno. Mti uliochanganyikana. Loo! mnasema, "Wao—wao wana mashirika makubwa. Wao—wao—wao—wao wanasaidia jambo *hili*. Na Msalaba Mwekundu unakubaliana na jambo hilo. Na mashule yote, wao. . . . Angalieni hapa!"

Loo! lakini kana tu Neno moja, hivyo ndivyo tu unavyopaswa kufanya upate kufa; hata jambo liwe ni la kiakili namna gani, ni zuri namna gani. Yesu alisema, "Chachu kidogo hulichachusha donge zima." Doa moja la chachu huharibu donge zima. Neno moja la Mungu, likiwekwa mahali pasipo, huharibu picha yote. Vipi mkono wangu ukiwa mahali mguu wangu unapopaswa kuwa? Mnaona? Vipi kama sikio langu lingalikuwa hapa chini ambapo mkono wangu unapaswa kuwa? "Chachu kidogo huchachua donge zima."

Unasema, "Unajuaje jambo Hilo ni kweli?" Mungu hulithibitisha kuwa ni kweli. Yeye hulithibitisha. Yeye alisema

jambo Hilo hapa katika Neno, halafu analithibitisha. Hivyo ndivyo tunavyojua ni kweli ama si kweli.

Kukana Neno moja tu ndilo linahitajika upate kufa. Kulisababisha matokeo yale yale katika wakati huu mwovu, mauti ya rohoni, kama kulivyoleta mauti ya kimwili kwa jamii yote ya binadamu.

116 Angalia jinsi Shetani alivyokifanya wakati huo wa kisayansi kule nyuma, cha Nuhu, kutegemea akili zao wenyewe. A-ha! Biblia inatwambia, katika Zaburi, "Tusizitegemee akili zetu wenyewe." Na, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na la Mungu liwe kweli." Lakini Shetani, kwa maarifa yake, tangu mwanzo kwenye bustani ya Edeni, aliwafanya watu kutegemea akili zao wenyewe. Na, mwajua, kwa viwanda vyake vikubwa vya Max Factor alivyokuwa navyo kule nyuma, aliwafanya wanawake kuwa warembo sana hata ikamsababisha mwana wa binadamu. . .wana wa Mungu, hasa, kuanguka dhambini na kuwaoa. Yeye. . . Wanawake walikuwa warembo sana, wenye sura nzuri sana.

117 Sasa mchukue mwanamke wa kawaida mitaani leo. Wengi wenu wamesoma hadithi hiyo; hamjapata kusikia, maana ni ya zamani. Pearl O'Brien, ni wangapi walipata kusikia habari zake? Hakika. Yeye alidhaniwa kuwa mwanamke aliye mrembo kuliko wote duniani. Mbona, hakuna mtoto wa shule anayeenda shuleni leo ila aliye mrembo mara mbili ya vile yeye alivyokuwa. Ni kwa nini? Urembo wa wanawake utatukia katika siku za mwisho.

Wao wamekata nywele zao. Wanawavalisha nguo ndogo za wasichana wadogo. Wanavaa kaptula, na bikini, na sijui mnaziitaje, wanazivaa. Wanajipodoa, na rangi ya midomo, na mambo haya yote ya kila namna, kuwafanya kitu wasicho. Mnaona? Bali kwa maarifa ya kisayansi wameweza kufanikiwa kufanya jambo hili. Je! mnajua kuna fedha nyingi zinazotumiwa kwa vipodozi vya wanawake, kuliko ilivyo matumizi, katika Marekani, mara mbili ama tatu zaidi, katika chakula tunachokula? Thibitisha jambo hilo, hiyo ni kweli, kwa ajili ya vipodozi.

118 Angalia, "Wana wa Mungu waliwaona binti za wanadamu," si binti za Mungu, "binti za wanadamu, ya kwamba walikuwa wazuri," na ikawafanya wana wa Mungu kuanguka katika upotovu huu. "Na wakawachukua wanawake wa aina hiyo na kuwaoa," na jambo hilo likasababisha wakati wa ukahaba, kama tu ilivyo siku hizi; kama ilivyokuwa Sodoma, kama ilivyobashiriwa itakuwa siku hizi.

Hiyo, wakati wanaume na wanawake wa siku hizi wanabadilishana wake. Kama hawamtaki mke huyu, wao—wao wanaenda huko Reno, Nevada, na kuoa; na, ama kupatia talaka, huyo, na kuoa tena katika dakika kumi na tano. Nao wanawake ni warembo sana hata karibu ni vigumu kujizuia

kwao. Na ni kitu gani? Ibilisi! Mnamwona Shetani akiwa angali katika urembo? Angalieni.

119 Angalieni, wao hawakusamehewa hiyo dhambi. Wakati huo mrenbo wa kisayansi ndio wakati ule ule mwovu ambao Mungu aliuangamiza akauondoa juu ya uso wa dunia; wakati huo wa mrembo, wa kisayansi. Yesu alisema itakuwa hivyo tena kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Hiyo ni kweli? Angalia, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu," wakati hao wote walipojaribu kuoa... Sasa angalia, "Wana wa Mungu waliwaoa binti warembo wa wanadamu," wala Mungu kamwe hakuwasamehe jambo hilo.

120 Ni kama tu vile vile mafundisho ya Balaamu, kwamba yeye alisababisha hao wanawake warembo, wenye akili na wa kisayansi wa Moabu ku-...wakiwa na macho yao matamanifu, rangi zake na poda, manukato yake mazuri, kuwavutia wana wa Mungu; dhidi ya wanawake wao wenyewe waliofanya kazi na waliokuwa na sugu mikononi mwao, wasiojipodoa. Wakawavutia, na "Hebu tuoane, kwa maana sisi ni wa jamaa moja." Huo ulikuwa ni uongo! Ulikuwa ni—ni uongo, na kazi nzuri ya ibilisi, kuwafanya wana wa Mungu kuoa bi—binti za wanadamu.

Ulikuwa ni uongo wa ibilisi, kwa Balaamu, yule nabii wa uongo, kujaribu kutabiri dhidi ya Musa aliyejaribu kushikilia jamii hiyo pamoja; kusema, "Vema, sisi tunaamini Mungu yule yule. Tunatoa dhabihu ile ile. Tuna dhabihu zile zile. Tunafanya kila kitu namna ile ile."

"Watafanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Mnaona? [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Tokeni kwake, enyi watu! Hamna uhusiano wo wote naye!

121 Angalia, haikuelekea kwamba Mungu angefasiri Neno Lake kwa wakati mwovu wa Kaini. La. Mungu hangeweza kuwafasiria Neno Lake. Angalia... [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.]

Mungu, yale maarifa ya kuufanya ulimwengu uwe wa kupendeza sana na wa kisayansi na wenye dhambi, ilimbidi Yeye kuuangamiza? Hivi Mungu angefanya jambo hilo, kufanya ulimwengu wa kupendeza sana, angalia hapa, Mungu akiwafanya binti Zake warembo sana, na angewavalisha kizinifu sana, hata wanawe wangewatamani na kufanya uzinzi? Ati nini? Ati Mungu afanye jambo kama hilo?

Kundi hili uchi, lililovua nguo la Walaodikia, wakimwabudu Mungu wa ulimwengu huu, kupitia elimu yao ya maadili, na elimu, na werevu, na urembo! "Tokeni kwake," Biblia ilisema, "msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake." Mungu atanyesha mvua ya mawe kutoka mbinguni siku moja, ukubwa wa ratili mia kila moja, na atamwangamiza yeye kwa kumpiga

yeye na mawe; kama Neno Lake daima lilivyosema Yeye alifanya, sheria Zake.

Vema, kama Mungu alifanya jambo kama hilo, akawafunulia watu kama hao Neno Lake, Yeye angekuwa— angekuwa anavunja kusudi Lake Mwenyewe. Mungu si mjinga. Yeye ni chemchemi ya hekima yote.

Kwa hiyo unaona mahali upuzi huo ulikotoka? Ulitoka kwa Shetani, na ungali ni wa Shetani. Na kanisa limeamini jambo hilo.

122 Sasa mnaona, enyi wanawake, ninajaribu niwezavyo kuwaonyesha Neno la Mungu. Biblia ilisema, "Mwanamke akikata nywele zake, yuaabisha kichwa chake," ambacho ni mume wake. Na mume wake ndiye kichwa, pamoja na Mungu, kwa hiyo yeye anamwaibisha Mungu pamoja na mumewe.

123 Sasa jambo hili linaonyesha kichwa cha utaratibu huu wa kanisa la ulimwengu ni nani. Hilo linaonyesha kichwa chake ni nani. Ni Shetani, katika mfano wa mtu maalum, mtu wa maarifa, maarifa maalum. Yeye anajua zaidi ya hao wengine wote. Haidhuru Neno linasema nini, yeye—yeye ana fasiri yake mwenyewe ya Hilo, mnaona, fasiri kwa wakati huu mwovu.

124 Angalia mipango yake kujenga kanisa maalum la kimadhehebu, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, mnaona, madhehebu maalum, ili kwamba ulimwengu wote umwabudu, yule mnyama, chini ya jina la muungano wa Ukristo. Je! mngetaka kusoma jambo hilo katika Biblia? Ufunuo 13:6 na 8. Ni mnara wa kisasa wa Babeli.

125 Hivi hamkumbuki jinsi ambavyo Nimrodi, yule mnafiki, alivyojenga huu mnara mkubwa na kuifanya miji mingine yote midogo kumpa ushuru? Babble na Babeli ni kitu kile kile. Huo hubadilisha tu majina yake, na, jinsi unavyojitokeza. Huo ni, Rumi sasa ni Babeli. Na ulimwengu mzima umeletwa Babeli, na umeletwa na Baraza la Makanisa Ulimwenguni ambalo litamfanya kila mtu alisujudu. Nawe umechukua alama ya mnyama, bila kujua ulichokuwa unafanya. Kwa sababu . . .

Bali wale walioteuliwa watalisikia Neno na kutoka kwake.

126 Jinsi madhehebu yalivyo kinyume cha Neno la Mungu! Yeye kamwe hajakuwa na moja, hajajishughulisha na moja kamwe, na kamwe hajashughulika na moja. Ninataka wanahistoria wanionyeshe mahali po pote ambapo nabii aliyepata kutokana na kanisa. Nionyeshe mahali ambapo Mungu aliwahi kubariki kanisa ambalo lilikuwa . . . baada ya kufanyika madhehebu. Liliwekwa kwenye rafu na likafa, likiwa na hekima ya akili kutoka kwa ibilisi, kwa viongozi wao, na limekataa Neno la Mungu lilipokuwa linakua kufikia kiwango kikamilifu cha Kristo. Sasa limefikia kileleni. Ni tofauti jinsi gani!

Jitengeni na huyo Hawa asiyeamini, enyi wana wa Nuru ya jioni!

127 Shetani, mungu wa wakagi huu, kwa maarifa yake, akiwafanya watu kula kutoka kwenye mti wake uliochanganyikana wa mema na mabaya. Angalieni, Shetani, kwa maarifa yake, akiwafanya watu wa wakati huu mwovu kula kutoka kwenye mti wake wa mema na ubaya. Yeye anasema ya kwamba anajenga ustaarabu mkuu zaidi wa Kikristo, kwa maarifa yake ya mema na mabaya, ustaarabu mkuu zaidi ya wa Kikristo.

128 Lakini maskini Bikira wa Kristo, Neno, Kundi, Bibi-arusi, hayajali maarifa ya shetani. Yeye huninii, huyo, hujitenga naye. Ni nini. . . Sasa hebu tuzungumze juu Yake, kwa muda kidogo. Yeye humngojea Bwana Wake na fungate Yake ya ule Utawala wa Miaka Elfu, kweli, pamoja na Bwana Arusi Neno, kwa kuwa Yeye ni Bibi-arusi Neno.

129 Maarifa na ustaarabu, na Ukristo wa kweli, havina uhusiano. Ustaarabu, na Ukristo wa kweli, havina uhusiano kamwe.

Ustaarabu ni kwa maarifa. Sote tunajua jambo hilo. Na maarifa yanatoka Edeni, alithibitisha jambo hilo, kwa yale aliyohubiri Edeni. Na maarifa husababisha mauti. Hiyo ni kweli? Ni kitu gani kilichosababisha mauti katika bustani ya Edeni? Maarifa. Lakini hayawezi kuwa ni ya Mungu, kwa hiyo ni ya ibilisi. Whiu, je! hilo si lilikuwa zuri! Maarifa, sayansi, elimu, ndicho kipingamizi kikubwa sana alichopata kuwa nacho Mungu. Ni ya ibilisi.

Sasa nitapata barua kwa ajili ya jambo hilo, ninajua. Ninazingojea.

130 Angalia utamaduni ulikotufikisha sasa. Mnaona? Angalieni yale umefanya. Tuko wapi? Tumeegemea vitu hivyo, kupitia akili yetu wenyewe kwa sayansi.

Mnasema, "Na Mungu je! unafikiri Yeye hajui?" Loo! la.

Mungu ataanzisha aina Yake Mwenyewe ya ustaarabu duniani, wakati atakapochukua mamlaka. Huu ni ulimwengu wa Shetani; yeye ni mungu sasa wa ulimwengu wake wa maarifa ya kisayansi. Lakini Mungu ataanzisha aina Yake Mwenyewe ya ustaarabu. Hautakuwa ustaarabu kama huu. Kumbukeni tu jambo hilo. Hautakuwa aina ya ustaarabu kama tulio nao leo. La, la. Utakuwa ni wa kulingana na Neno Lake na kusudi Lake. Kwa kuwa, mungu wa wakati huu mwovu wa sasa ataangamizwa, na ufalme wake pamoja naye.

131 Wakati huu wa kisasa unaopenda maarifa haungeweza kuwa na kiongozi bora kuliko yule uliye naye, Shetani, mpotoshaji wa Neno la Mungu, kama alivyoanza katika bustani ya Edeni, lakini ni mtu wa dini anayetegemea akili yake mwenyewe.

Kama nilivyosema hapo awali, Mithali 3:5, ya kwamba, "Hatupaswi kutegemea akili zetu wenyewe."

Hawana budi kuwa na mungu, kwa maana wao ni wanadamu. Hata hivyo, yeye huwatengenezea kile wanachotaka. Kama ilivyokuwa binadamu, daima, binadamu wote . . . Tulipokuja hapa, tuliwakuta Wahindi pia wakiabudu sanamu, na jua, na kila kitu. Kama mwanadamu, hawana budi kuwa na mungu. Kwa hiyo wakati huu mkuu wa bongo hauna budi kuwa na mungu, kwa hiyo umekuwa . . . Mungu wa dunia hii amekuwa maarifa, madhehebu, sayansi, "wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake."

132 Angalia, mungu wao huwafanyia kile tu wanachotaka. Wao wana tamaa ya mwili, na huo ndio anaowapa. "Wanataka kuvaa bikini. Waache wazivae. Kama wanataka kufanya jambo *hili*, ama *lile*, waache walifanye. Halina madhara; wao wanaenda kanisani. Mama yao alikuwa Mmethodisti, Mbatisti, Mpentekoste, Mpresbiteri. Waache tu."

Huyo ni mungu wa wakati huu; mwerevu, mwenye hekima, wa kisayansi. Hilo halihitaji imani. Si lazima kuthibitisha cho chote. Tayari limethibitishwa, na maarifa yao. "Vema, sisi ndilo kanisa kubwa sana lililopo mjini," maarifa yao. "Mchungaji wetu ana D.D., Ph.D." Mnaona, hawahitaji imani yo yote; wanategemea maarifa. Anawaacha waishi namna yo yote, mradi tu wanakuja kumwabudu kwa madhehebu yao na kanuni za imani. Kuna jicho kubwa jeusi pale, lakini liangalie.

Wanalicheka Neno la Mungu, wakisema mambo yaliyo kinyume na Neno; na kujaribu, kwa maarifa yao, kuthibitisha kisayansi ya kwamba Neno si kweli. Loo, tunaishi katika wakati wa namna gani! Mnaona Mungu wa wakati huu?

133 Angalieni, lakini Mungu anangoja mpaka uovu wa hawa Waamori wa kisasa ujazwe. Msijali, Yeye atakuwa amemtayarisha Musa wake wakati huo. Kutakuweko na kutoka, siku moja, kuelekea kwenye nchi ya ahadi. Musa atatokea, atakayewaita watoke, "atakayeirudisha Imani ya watoto iwarudie baba zao." Itakuja, moja ya siku hizi. Haikuninii . . .

Mnasema, "Vema, angalia jinsi tunavyofanikiwa."

Hakika, uovu wa Waamori haujatimia bado. Utakuja, moja ya siku hizi. Waache wajiangamize wenyewe.

134 Ustaarabu, maarifa, hupotosha Neno la Mungu wapate kuridhisha ladha yao wenyewe. Kila madhehebu hufanya jambo lile lile. Shetani basi anahubiri injili yake mwenyewe ya maarifa katika kanisa lake mwenyewe.

135 Kuna tabaka mbili tu za watu zilizonenwa katika Agano Jipya. "Wana wa Mungu, na wana wa ibilisi." Mlijua jambo hilo? Mnataka kuandika Andiko lake? Yohana wa Kwanza 3:10,

kama mkitaka Maandiko. Ninalisoma papa hapa, nimeliandika. Vema. Vema.

136 Katika Waefeso 2:2, wao wanaitwa, “Wana wa kuasi.” Kama Hawa alivyokuwa, waasi wa Neno la Mungu. Wana wa kutii, na kuasi, hawana uhusiano.

Basi Bibi-arusi wa Kristo anawezaje kuhusika na madhehebu, wakati mmoja hatii na mwingine anatii? Moja lawezaje, kuwa Neno; na hilo lingine, neno lililopotoshwa? Kahaba na mwanamke safi wanawezaje kutembea pamoja katika mapatano? Hawawezi kufanya jambo hilo. Hawana ushirika wo wote. “Tokeni kati yao!” Ni jambo la ibilisi. Ni alama ya mnyama. Yanaelekea moja kwa moja kwake sasa; madhehebu yote. Sijali ni ya nani.

Mungu anachukua, si madhehebu, “watu kwa ajili ya Jina Lake.” Madhehebu hayatapokea Kweli hizi. Itachukua mtu binafsi ambaye anaweza kumwona Mungu, kuangalia Neno Lake na kuliamini, na asiwe mfuasi madhehebu yo yote; bali amwishie Mungu, si kwa ajili ya madhehebu yake, hekima ya kiakili aliyofundisha askofu fulani ama kitu fulani kilichofundisha hilo. Hiyo ni kweli.

137 Wana wa kuasi, na wana wa kutii, hawana uhusiano wo wote. Mmoja wa. . .ni wa siku ya Nuru; mwingine, wa usiku na giza, wakati mwovu, wakati huu mwovu wa giza, vilabu vya usiku, madansi, hata hivyo ni mshirika wa kanisa. Ni sawa kwa mungu wao. Hawana hukumu yo yote juu ya jambo hilo; hakuna kinachowasumbua.

“Mbona, hainihukumu kukata nywele zangu,” mwanamke fulani alisema. “Halisumbui dhamira yangu.” Yeye hana dhamira zaidi ya vile nyoka asivyokuwa na kiweo. Hiyo ni kweli. Bila shaka hana. Hajui dhamira ni nini. Imekaushwa sana hata hajui ni nini. Hiyo ni kweli.

138 Wakikanyaga kila mahali, juu ya Neno la Mungu, wakisema, “Mbona, huyo ni mzee mjinga. Usiende kule; wao ni kundi tu la makelele na kupiga mayowe, hata hivyo.” Hawajui zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhottentoti asivyojua hadithi za Kimisri. Hiyo ni kweli. Ni kweli.

“Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. Kwa maana hawa ndio wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga.”

“Jamani! mpenzi, unaninii, unapaswa kufanya jambo *hili*. Jamani! mpenzi, nafikiri maskini mhubiri wenu mjinga pale, kama ukininii tu. . .Jamani, ungeonekana mrembo katika ‘kini,” ama cho chote unachokiita kitu hicho. “Wewe, kama ungefanya yote *haya*, *yale*, na yale *mengine*. Mbona, sigara ndogo haitadhuru mtu ye yote. Mimi ni mfuasi wa kanisa, nawe unajua madhehebu yetu yenaheshimiwa kama ya mtu mwingine

yule.” Usimwamini huyo mwongo wa kale aliyepakwa rangi. Anakudanganya. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

139 Ni sawa kwa mungu wao. Loo! yeye anafikiri jambo hilo ni zuri sana, nao wanampenda sana kwa ajili ya hilo.

Jamani, watabishana nawe. Watasimama moja kwa moja na kubishana juu ya jambo hilo. Mbona, hakika, Shetani alisimama moja kwa moja mbele za Yesu Kristo, Neno, na kujaribu kusema, “Imeandikwa.”

Na Yeye alikuwa hapo, Neno la Mungu lililothibitishwa. Akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani!” Kaenda tu na kufanya vivyo hivyo.

Ni kama vile jamaa fulani alivyoniambia wakati mmoja, kasema, “Sasa, kama unaamini ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kweli, nawe unaamini unao Huo,” kasema, “sasa nipige kwa upofu.” Huyo alikuwa ni mhubiri. Kasema, “Nipige kwa upofu!” Akasema, “Paulo alimpiga m—mtu kwa upofu siku moja.”

140 Nikasema, “Bwana, ninawezaje kukupiga kwa upofu wakati tayari wewe ni kipofu? Ninawezaje kukuua wakati tayari umekufa?”

Akasema, “Mimi, macho yangu ni ishiri kwa ishirini!”

Nikasema, “Sehemu yako ya kimwili; bali ungali ni kipofu.”

“Haiwezekani! Biblia haifasiri mambo. Sisi hunena mahali inaponena Biblia, na kunyamaza mahali inaponyamaza.”

141 Nikasema, “Vema, wakati Eliya aliposhuka hu—huko Dothani, mnaona, jeshi lote la Ashuri liliwazingira. Ndipo mtumishi akakimbia, akasema, ‘Ole wetu! baba yangu!’ Kasema, ‘Baba yangu,” kasema, ‘Waashuri wametuzingira.’

“Eliya akapangusa macho yake, akaamka na kusema, ‘Kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.’

“Akasema, ‘Sioni mtu ye yote.’

“Kasema, ‘Mungu, yafumbue macho yake.’ Sasa, yeye alikuwa kipofu. Ndipo akaangalia pande zote za yule nabii mzee, na juu ya milima; kulijaa Malaika, na magari ya Moto, na farasi wa Moto.

“Naye akatoka akaenda kule nje, na Biblia ilisema,‘Akawapiga kwa upofu.’ Upofu kwa kitu gani? Kwake. Akaondoka, akasema, ‘Ati mnamtafuta Eliya?’

“‘Naam, tunamtafuta.’

“Kasema, ‘Njoni, nitawaonyesha mahali alipo.’ Eliya akiwaongoza kwa Eliya. Vipofu!”

Nikasema, “Unajua nitakachokwambia? Vile vile tu Bwana wangu alivyomwambia baba yako, ‘rudi nyuma yangu.’” A-ha. A-ha.

142 Angalia, wana wa kutii, na kuasi, hawana uhusiano wo wote. Wa kuasi humwabudu mungu wao. "Loo!" wao wanasema, "tunaamini Biblia." Naam, ni mti wa mchanganyiko. Mnaona, wao wanaongeza ulimwengu na maarifa Kwake. Mti wa Shetani, uliochanganyikana; mnaona, yeye alikula kutoka kwenye mti wa Shetani, mema na mabaya. "Loo, tunaamini Neno." Hakika, bali si lote. Hawa aliamini Neno, pia, lakini akamwacha—akamwacha Shetani achukue mti wake na kulipotosha kidogo. Hivyo ndivyo ilivyo.

"Ye yote atakayeongeza neno moja, ama kuondoa Neno moja Kwake." Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Angalia. Vema.

143 Wakati huu mwovu ni wa giza, hata hivyo ni mfuasi wa kanisa. Mungu wao, wanampendea jambo hilo, yale anayowaruhusu kufanya. Hajisikii kuhukumiwa. Hakuna kinachowasumbua mradi tu ni wafuasi wa kanisa.

Balaamu alilifundisha kanisa jambo lile lile. "Na tuungane; sisi sote ni kitu kimoja." Huo ulikuwa ndio ujanja wa mwisho. Mungu hakuwasamehe kamwe kwa kuamini uongo kama huo.

144 Kumbukeni, ilikuwa ni dhambi isiyosameheka, mara tatu katika Biblia, kwa mtu ye yote kuongeza neno moja la ufasiri wao wenyewe kwenye Neno la Mungu baada ya Hilo kuthibitishwa kwamba ni Kweli.

Katika bustani ya Edeni, moja kwa moja, katika bustani ya Edeni, neno moja lililoongezwa lilisababisha mauti.

Wakati Balaamu alipoongeza neno, ya kwamba, "Sisi ni mmoja," wao, Mungu hakuwasamehe Israeli jambo hilo. Kila mmoja wao aliangamia jangwani, isipokuwa wale watatu ambao Mungu aliwatoa.

Yesu alisema, "Hao, kila mmoja wao, amekufa," hiyo ni kutengwa Milele. Wote wameangamia; hawakusamehewa kamwe. Ni dhambi isiyosameheka; hawakusamehewa. Loo, jamani!

Ikimbieni, enyi watoto wa Nuru za Jioni!

145 Mnaona sasa ni nani kiongozi wa wakati huu mwovu wa kisasa na wa kidini? Ni ibilisi, akichukua huo mti wa mema na mabaya, na kuuweka huko nje, angalieni, akimleta bibi-arusi wake anayevutia wa kanisa kwenye baraza la ekumenia kwa ajili ya arusi. Hilo ni zuri. Kanisa lake linalovutia la kisayansi, likiwa na ma—ma—madigrii yote yanayoweza kuchukuliwa; zile Ph.D. kutoka katika kanisa la Kristo, Ph.D. kutoka la Kibatisti, Kipresbiteri, Kipentekoste, na wote. Wakizileta zote, pamoja na mavazi yao yaliyopambwa na makanisa makubwa, yote kuelekea baraza la ekumenia, "Sisi ni mmoja." Wao hawatasamehewa jambo hilo kamwe. Madhehebu fulani, kuvaa chapa ya madhehebu, ni alama ya mnyama. Tayari

tumepitia jambo hilo hapa; kufanya jambo hilo. Yakimbieni, enyi watoto, yakimbieni! Mnaona? Kanisa kubwa linalovutia likienda kwenye arusi ya ekumeni, likivaa alama yake!

Kaptura, hakika, mavazi ya kilimwengu, ya zinaa, rangi, ni wanafunzi wazuri kweli wa ibilisi, kuwanasa wana wa Mungu; kumwoza mvulana mzuri mwenye malezi mazuri kwa baa la kale kama hilo. Hiyo ni kweli. Ni ninii jinsi gani . . .

146 Ulisema, "Kukata nywele, hilo lina uhusiano gani na jambo hilo?"

Ndugu, hebu tusimame hapa kwa dakika moja. Ninasikia tu mtu fulani akichukizwa na jambo hilo. Huenda ilikuwa huko nje kwenye simu mahali fulani.

Sikilizeni. Nywele kwa mwanamke ni nadhiri ya Mnadhiri. Nywele kwa Samsoni ilikuwa nadhiri ya Mnadhiri. Na hapo mwanamke anapozikata nywele zake, yeye—yeye hukana kabisa nadhiri yake ya Mnadhiri ya kwamba yeye ni Bibi-arusi wa Kristo. Kwa sababu, hapo, jambo hilo moja, yeye anaharibu Picha yote. Kweli! *Mnadhiri* ni "mtu aliyewekwa wakfu kwa kusudi fulani." Hiyo ni kweli? Samsoni alikuwa amewekwa wakfu kwa ajili ya wakati fulani kusudi fulani, kwa hiyo alikuwa na nywele ndefu. Mwanamke ambaye ni mwana wa Mungu, huachilia nywele zake zikue, kuonyesha ya kwamba yeye amewekwa wakfu kwa ajili ya kila Neno la Mungu.

147 Kama akizikata, sijali anacheza-cheza kiasi gani, huimba, yuko kwenye kwaya, hunena kwa lugha, hukimbia huku na huko, ama ana kila namna ya mashirika ya kutoa misaada, yeye amekufa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, Neno la Mungu. Wakorintho wa Kwanza 14. Yeye amekana nadhiri yake ya Mnadhiri na kujiuza kwa mungu wa wakati huu wa kisasa. Anafanya hivyo. Sasa, ni aibu kwako, ewe bibi, ama mwanamke!

148 Ni wanasa wana wa Mungu kweli, kama ilivyokuwa. Kama Yesu alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wanawake wazuri, na wana wa Mungu wakaanza kuoa miongoni mwao, ndivyo itakavyokuwa wakati atakaporudi Mwana wa Adamu." Na mungu wao anafikiri ni maarifa ya kutukuka, na ya kuvutia, na ya kisayansi. Mtindo wa Hollywood, ulioundiwa kwenye duka lake mwenyewe, hakika, hizi zote hapa zinazobana na upuuzi, mwajua.

149 Nalo, kanisa lake, kweli linapenda jambo hilo! Loo, jamani! "Ninataka ujue, mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mchungaji wetu ana akili ya kutosha hawezi kusema jambo kama hilo." Hana akili ya kutosha kusema mambo anayosema Mungu basi. Mnaona?

150 Yeye, kanisa, kweli linapenda sana jambo hilo. Linalipenda. Ni yale tu liliyotaka! Yeye hatajiunga na cho chote, ndugu, ama kuja katika cho chote kitakachombidi kutenda kama kitu tofauti

na Mayezebeli hawa wa kisasa walivyo, kwa kuwa hiyo ndiyo asili iliyo ndani yake.

Unawezaje kuwa na tabia nyingine yo yote. . . "Ni yupi akijisumbua aweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja?" Kama ulizaliwa uwe na urefu wa futi tano, hutakuwa futi sita. Loo! naam, kama "mtambo wa kutanua" wa Booth-Clibborn.

151 Basi sikiliza, ewe mwanamume, enyi kundi la akina ricky! Kama ulizaliwa kuwa mwanamume, basi enenda kama mwanamume. Hizi nywele ndefu zinazoning'inia usoni mwako, na zimesokotwa kama mambo ya zinaa, mbona, enyi kizazi cha nyoka kilichopotoshwa! Mna nini, hata hivyo?

Mungu wangu atalihukumu taifa hili siku moja kwa moto. Yeye atalizamisha chini ya bahari. Saa ya hukumu Yake imekaribia. Ulimwengu mzima utaangamizwa.

152 Upotovu wa dini! Upotovu wa kibinadamu; wanaume hata hawajui wao ni wa jinsia gani, wala wanawake hawajui. Wanasimama na jozi ya ovaroli ya mwanamume, ama jozi ya maskini kaptula ndogo, nguo ambazo. . . kila hatua yake na umbo la mwili wake, na kujiita Mkristo. Yeye hata si bibi, sembuse Mkristo. Yeye ni kahaba wa mitaani anayetumiwa na Shetani, anaongozwa na Shetani, kuwapeleka wana wa Mungu jehanum, kutimiza Neno ambalo Yesu Kristo alisema lingetukia. Sikumaanisha jambo hilo, bali Yeye alilisema, hata hivyo. Mnaona mahali roho hii ya kidini inakotoka? Ule mti uliochanganyikana.

153 Mnasema, "Hizo suruali fupi zina ubaya gani," ama vyo vyote wanavyoziita, "visukuma pedeli, ama cho chote kile?"

Biblia ilisema, ya kwamba, "Mwanamke ye yote atakayevaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo mbele za Mungu." Hilo ni BIBLIA YASEMA HIVI.

Na mwanamke ambaye atakata nywele zake, huaibisha kichwa chake. Na hata. . . Ni dhambi kwa mwanamke kuomba akiwa na nywele fupi, Biblia ilisema hivyo, kuomba mbele za watu huku hakufunikwa kichwa chake. Na ninii zake. . .

Loo! unasema, "Mimi huvaa kofia."

154 Ewe mnafiki, ati unawafundisha hao wanawake mambo kama hayo! Wakati, Biblia ilisema, "Amepewa zile nywele ndefu ili ziwe badala ya mavazi," si baadhi ya kofia za kujitengenezea. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Mimi sihusiki; ninahusika tu na kuwaambia Kweli. Msiwe wasio waaminifu, kama Biblia ilivyosema, "Kulichanganya Neno la Mungu na uongo," ku—kufanya ama—ama kutimiliza matakwa ya kundi la akina riketa.

155 Nina neno *uovu* hapa. Nimeandika *evil* badala ya "Elvis." Yote ni karibu sawa. Neno *Elvis* linamaanisha "paka," na neno *Ricky* linamaanisha "panya mdogo." Unaposema "Ricky

mdogo," unamaanisha, "panya mdogo." Unavyomwita, hivyo ndivyo alivyo. Kama mtoto wako anaitwa hivyo, libadilishe upesi, kwa ajili ya Injili. Usimwite mtoto . . .

Hujapata kusikia majina kama hayo huko nyuma katika Biblia, ama katika wakati mwingine wo wote. Ni wakati, ni jina kwenye wakati huu. Kama kulipata kuweko na panya na paka waliopotoshwa, wako pale.

156 Yote haya . . . ? . . . vifaa vya muziki za dola milioni moja, na hawa watoto wakitembea hapa nje, hawawezi hata kwenda—kwenda shuleni bila kidude kinachoning'inia sikioni mwao, na maskini redio ndogo mfukoni mwao, ikienda, "buum-bu-buum."

Loo, walikuja kule nyumbani, nasi tukatengeneza . . . Hao jamaa waliokuwa wakijaribu kupaka nyumba yangu rangi kule. Tukasema, "Ondoeni kitu hicho hapa. Kama hamwezi kufanya kazi bila ya hicho, basi acheni kazi. Kinanifanya kuwa na wasiwasi sana hata siwezi kusimama karibu na hapa. Tumepaweka mahali hapa wakfu kwa Mungu. Hatutaki upuzi wa muziki wa namna hiyo wa siku hizi za mwisho mahali hapa." Nikasema, "Ifungeni la sivyo mwache kazi!"

157 Angalieni, wa kidini, hata hivyo, loo, hakika, wanaenda moja kwa moja kanisani na kusimama sebuleni, wakisikiliza muziki wa kipuzi.

158 Pia, angalia, Bibi-arusi Neno wa Kristo anaelekea kilele, pia. Tunapoona mahali mpinga-Kristo anakoelekea, alivyoanzia kule nyuma na sasa anafikia kwenye kilele; baraza la ekumenia litaliweka chini ya kiongozi wa kanisa. Na lile Kanisa dogo lililokuja moja kwa moja, pia, Bibi-arusi Neno wa Kristo kote katika nyakati, anafikia Kileleni, maana Yeye ataunganishwa tena na Mwenziwe. Daima, kama vile tu kanisa na cho chote kile, havina budi kuungana. Ile Ngano, cho chote kile, inavyorudi moja kwa moja kwenye kilele chake ilikoanza; kama vile Kaini na Habili. Bibi-arusi Neno akifikia kilele chake katika Utu wa Neno la Mungu lililodhihirishwa katika wakati huu mwovu tunamoishi. Mnaona mahali linakoelekea?

159 Naye Shetani hivi karibuni atamchukua bibi-arusi wake wa kielimu na kumwinua huyu mtu mkuu, ambaye ni mpinga-Kristo, ule uongozi wa kikanisa, na kumweka juu ya kiti cha enzi, "na dunia yote itamstaajabia yeye."

Ndipo Kristo atakapokuja. Na hao wawili hawawezi kuishi wakati ule ule. Ndipo ufalme wake utakapotwaliwa; yeye ataangamizwa.

Naye Kristo, Neno la Mungu . . . Ambalo, mwanamke ni sehemu ya mwili wa mwanaume. Wao si wawili; wao ni mmoja. Na Bibi-arusi, Kanisa, Neno, "watu walioitwa kutoka *hapa* na *pale*, kwa ajili ya Jina Lake," wataungana katika Mwili wa Yesu Kristo.

Nao ufalme wa mpinga-Kristo utatwaliwa na kuangamizwa. Ndipo Kristo atakitwaa kiti cha enzi, na kuketi kwenye kiti cha enzi cha baba Yake Daudi, na kutawala juu ya nchi miaka elfu moja; kisha atalikabidhi Kanisa kwa Mungu, "bila waa wala ila." Naam!

160 Sasa angalia nywele zake ndefu, nadhiri ya Mnadhiri kwa Neno. Nitamwonyesha Bibi-arusi wa Kristo sasa. Tulimwonyesha mpinga-Kristo, mahali alipo, wa dini na kadhalika, sayansi. Sasa maskini Bibi-arusi wa Kristo aliye mnyenyekevu anaamini tu Neno, hata awe ni Nani. Ni watu binafsi. Ninatumaini na kuamini ya kwamba kuna wengi walioko hapa wameketi, wengi wanaosikiliza. Na ninaamini ya kwamba mimi mwenyewe, na kila mmoja wenu ninyi nyote, ni sehemu ya Bibi-arusi huyo. Ninatumaini wengi. Na, itakuwa, wote waliochaguliwa kuwa huyo watakuwa huyo, maana ndiyo asili yao. Wao wanaona. Neno linaweza tu kutambua Neno. Haliwezi kutambua madhehebu au upotovu. Linatofautisha; Hilo ni Neno. Mnaona? Haliwezi kutambua cho chote . . .

Ngano haiwezi kuwa kitu ila ngano. Ilianza, ngano; itaishia, ngano. Wala gugu haliwezi kuwa ngano, ingawa linatiwa maji na upako ule ule. Mnaona? Lakini hiyo si ngano. Kama nilivyosema hivi majuzi, juu ya ule mti uliokuwa na matawi mbalimbali.

161 Nywele zake ndefu, nadhiri ya Mnadhiri, zinaonyesha ya kwamba Yeye amemwekea Mungu nadhiri. Joho lake zuri la Neno Lake lililoahidiwa kwa ajili ya wakati ambao Yeye anaishi, aliloviringwa nalo, likimthibitisha pamoja na Yeye Mwenyewe, kwa Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa kuwa, Yeye ni sehemu ya Bwana Arusi Neno, mkweli Kwake kwa kila njia.

162 Sasa angalia. Kama mwanamke akitoka nje hapa naye ameolewa na mwanamume, na anatoka na kufanya mapenzi na mwanamume mwingine na anashiriki naye, na arudi kwa mumewe, huyo mume anapaswa kumfukuza. Hilo ni sawa? Anapaswa awe mwaminifu kwake, sababu amemwekea nadhiri.

Naye Bibi-arusi wa Kristo amemwekea Kristo nadhiri; Naye ni Neno.

Hata asikonyeze jicho upande ule mwingine, mwanamke hapaswi hata kumkonyezea jicho mwanamume mwingine. Hapaswi kufanya ishara zo zote, asionyeshe kuvutiwa ko kote naye, kwa maana yeye yakini ni bibi-arusi wa bwana-arusi mmoja.

163 Hatutaki yo yote ya miti yanu iliyochanganyikana, madhehebu yenu. Uwe mwaminifu kwa Kristo, aliye Neno. Yeye atalithibitisha kwamba ni kweli. La, bwana, si hata kuvutiwa ko kote kwa cho chote kinachohusu kufanya mapenzi naye, si kujiunga na makundi yake wala cho chote kile, ama kumwacha

akushike kwenye mikono yake ama kukushughulikia, ama—ama kuzungumza nawe juu ya jambo *hili*, jambo *lile*.

Unasikiliza Sauti moja tu. "Kondoo zangu wanaijua Sauti Yangu. Mgeni hawatam- . . . " Sauti Yake ni nini? Sauti ya mtu ye yote ni neno lake. Nalo ndilo Hili, Biblia, neno moja lisiongezwe Kwake au kuondolewa Kwake. Dumuni waaminifu tu kwa Sauti hiyo. "Mgeni hawatamfuata," madhehebu.

164 Kwa kuwa, Yeye ni sehemu ya Bwana Arusi, mwaminifu Kwake kwa kila jambo, akiingojea ile Arusi. Kuungana, si kwenye baraza la ekumenia; lakini hewani, kwenye Karamu ya Arusi. Yeye amekwisha pewa . . . Hili ni kwa ajili ya kanisa letu wenyewe. Yule . . . Yeye amepewa, na zimefunuliwa Kwake, zile siri za Muhuri Saba za Biblia. Mnaona? Yeye anaona ujinga wa yule mdanganyifu, akiwa karibu sana na ile Kweli, hata karibu awapoteze walio Wateule. Yeye analiona hilo. Bibi-arusi . . .

165 Mnaona zile roho mbili zinazopingana zikitenda kazi katika wakati huu mwovu? Mnaweza kuziona? Kila moja ni ya dini sana, Kaini na Habili, zile roho zikifikia vilele vyao tena, zingali vile vile zilivyoanza. Moja, ikiabudu kwa urembo, na kwa maarifa, na kwa elimu, na kwa sayansi, na kwa elimu ya maadili. Na Hiyo nyingine, kwa imani ya ufunuo wa Neno la Mungu. Zote mbili zimesimama katika jengo hili asubuhi ya leo. Hiyo ni kweli.

166 Ufunuo, ama imani, katika Neno Lake, havidai kuwa na maarifa; Mkristo halisi na wa kweli.

Wao wanasema, "Je! umepata, ama una shahada ya daktari?"

Hadai kuwa cho chote. "Ni—ninaamini Neno Lake." Mnaona? Hadai kuwa lo lote. Hadai kuwa na elimu. Si mfuasi wa madhehebu yo yote, chama cho chote, madhehebu yo yote. Yeye ni wa Kristo. Ni Mkewe; si mke kanisa.

Yeye ni kahaba. Biblia ilisema yeye alikuwa "kahaba," na, "MAMA WA MAKAHABA," nao wote wanaungana na kuunda kahaba yule yule. Na mwanamke wa ina hiyo ni mwanamke asiye mwaminifu kwa Mume wake; na anamdai Kristo kama ni mumewe, na ni mfuasi wa madhehebu. Upuuzi kama huo! Sisi ni mali ya Kristo.

167 Lakini, katika utii, maskini Mwanamke huyu wa imani, anayeishi kwa imani, Bibi-arusi; mtu huyo *hapa*, *pale*; hapa, ametoka mahali pengine; kanisa lingine, madhehebu mengine fulani, cho chote kile, katika ninii fulani . . . Anaamini Neno la Mungu, ni mtiifu, anangojea katika upendo, kwa ajili ya kuthibitishwa kwa ahadi ya wakati huu. Yeye anangojea jambo hilo. Yeye ni sehemu ya Neno hilo, Naye anangojea maisha Yake yadhihirishe hilo Neno.

Ndugu zangu, hivi hamwezi kuona jambo hilo? Natumaini hilo halikuwapita.

Mwili unangojea (ambao ni Neno), unangojea Uhai (ambao ni Roho) kuthibitisha ama kuufanya hai. Hicho ndicho anachongojea. Hakuna uhai mwingine unaoweza kutenda kazi ndani Yake. Huwezi kufufuka kwa njia nyingine yo yote. Hata hivyo, yeye huuhisi huko nje, na anajua litatukia; ndipo hili hapa linatukia, ndipo anaamka. Mungu alisema, "Na iwe," Naye akatokea kama yule wa kwanza alivyotokea.

168 "Wana wa kuasi" linamaanisha kutii . . . *Kuasi* maana yake "uhalifu." Nililiangalia hilo kwenye kamusi, nipate kuwa na hakika. Maasi, maasi dhidi ya nini (kitu gani?) Neno la Mungu lililofunuliwa. Kama Kaini alivyofunua . . . alivyoasi dhidi ya ufunuo aliofunuliwa Habili, uliothibitishwa na Mungu kwamba ni wa haki. Naye Kaini akauasi huo, na kumwua ndugu yake.

Mafarisayo, wakiwa na maarifa yao wenyewe ya kimadhehebu kuhusu Neno la Mungu lilivyokuwa, waliwachagua watu wa kujichagulia wenyewe, wakaliasi Neno la Mungu lililothibitishwa na kudhihirishwa kwa ajili ya siku hiyo, Yesu Kristo, na wakamwua. Hiyo ni kweli?

Hicho ndicho "wana wa kuasi walicho," ni maasi dhidi ya Neno la Mungu.

Sasa unaona mahali walipo?"Loo, siku za miujiza zimepita. Yesu Kristo si yeye yule bado. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Takataka zote hizo ni upuuzi!" Unaona, maasi! Si lazima waseme mambo mawili; inawapasa tu kusema jambo moja, yatosha. Hayo ni maasi, papo hapo. Hawawezi kusema huna macho, huna maskio; huna budi kuchukua mwili wote, Neno lote. Mnaona?

Roho Mtakatifu anaita, "Ondokeni kwake, msishiriki mafundisho yake ya sharti ya kimadhehebu," wakati anapocheka na kudharau Neno la Mungu la siku hii.

"Kwa maana Mungu hadhihakiwi," kumubukeni tu. Yeye atakiona. Usijali. Atakiona. Biblia, katika Waefeso 4:30, kama ukitaka kuandika jambo hilo, Waefeso 4:30, ilisema, "Mungu hadhihakiwi. Cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." Wao hawawezi kudhihaki na kufanyia mzaha, na kusema mambo haya, na kuepuka jambo hilo. "Kama mkate juu ya maji, watavuna."

169 Yeye ni bibi-arusi wa ibilisi, amevalishwa maarifa yake ya kidini, yanayopenda dhambi kwa ajili ya wakati huu mwovu wa sasa, kuwadanganya ninyi. Loo, jamani! Kundi zima ama madhehebu ya roho zinazoshawishi, kwa maarifa ya kisayansi na ustaarabu wa kisasa! Likidai . . .

Tutafunga katika dakika chache tu. Itanibidi kukoma, maana siwezi kumaliza yote, mnaona.

Akidai kwamba anajenga ulimwengu mzuri sana mpate kuishi humo. Yeye anadai, ya kwamba, katika ustaarabu wake, amejenga makanisa mazuri, vyuo, mashule, mahospitali, maktaba, na usaidizi wa muda wa mwanadamu, bila Neno la Mungu. Yeye amefanya jambo hilo. Amethibitisha ya kwama angeweza kulifanya. Nao watu wameliangukia; naam, bwana; mashule, madhehebu, utamaduni, watu waliovalia vizuri, watu waliolishwa vizuri.

Afadhali niwe kwenye mstari wa kuomba mkate, na kuwa sawa na Mungu; kuliko kula kuku aliyekaangwa mara tatu kwa siku, na inibidi kuwa mfuasi wa kahaba kama huyo.

170 Kumbukeni, saa imekaribia sana wakati alama itakapokuja. Utakuwa aidha ndani yake ama nje yake. Itakuja kama mwizi usiku. Itakukuta moja kwammoja hapo ndani, nawe uko hapo. Hakuna njia ya kutoka humo wakati huo; tayari umeipokea. Tokeni!

Malaika alishuka kutoka Mbinguni, akiwa na uso mkuu unaong'aa. Akawalilia watu kwa sauti kuu. Ikaitikisa dunia. "Tokeni Babeli, kwa kuwa umeanguka. Msishiriki mapigo yake, enyi watu Wangu!" Tokeni kwake. Tokeni! Hivi hatukulisoma katika Neno, muda kidogo uliopita? *Malaika* ni "mjumbe," mnaona, akishuka. Angalia Roho Mtakatifu, "Tokeni kwake, msije mkashiriki."

171 Sasa yeye amejenga mambo haya yote. Amejenga makanisa makubwa. Amejenga chuo, mashule, akiwachukua watu na kuwaelimisha kufikia, unavyoitwa, ustaarabu bo—bora zaidi. Nao wamewaelimisha kwa ustaarabu wa kisasa uliowaleta kwenye shimo la mauti, kwa maarifa, mbali na Mungu na Neno Lake.

Hivi hamwoni njama yote nzima? Mnaona jambo hilo, enyi kanisa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Huko nje hewani, kama mkiona jambo hilo katika makusanyiko yenu wenyewe huko nje, semeni "amina," waliosalia watajua mahali mnaposimama. Mnaona?

Yeye amefanya jambo hilo. Yeye ni . . . Ni mungu wa dunia hii, naye amejenga vyuo. Amejenga vyuo vikuu. Amejenga mahospitali. Amejenga maktaba. Amejenga vitu hivi vyote kwa ajili ya msaada wa muda wa mwanadamu, wa kutosha tu kuwadanganya, wapate kutoka kwenye hilo Neno. Naye amewaongoza kwenye kitu gani? Ulimwengu mzima wa makanisa umetumbukia mautini, kwa maana Mungu alisema ya kwamba angemchoma huyo kahaba, na watoto wake, kwa moto wa milele.

Tokeni kwake, enyi watu! Msishikiwe hapo ndani. Tokeni kwenye kitu hicho upesi mwezavyo!

Kwa maarifa yake ya kisayansi, yeye amefaulu kufanya jambo hili, sasa angalia, bila Neno la Mungu.

172 Mungu kamwe hakutuagiza tutoke twende tukajenge mashule. Kamwe hakufanya hivyo. Hakutuambia kamwe tujenge mahospitali. Hayo ni mema. Hakutuambia kamwe tujenge maktaba. La, bwana. Hakutwambia.

Yeye alisema, "Hubirini Injili." Na, Injili, ni kudhihirisha, kuonyesha nguvu za Roho Mtakatifu.

Paulo alisema, "Injili ilitujia, si kwa neno peke yake, bali kwa kudhihirisha na dalili za Roho Mtakatifu." Paulo alisema, "Sikuja kwenu kwa ufasaha wa maneno ya hekima ya daktari fulani na kadhalika, lakini nilikuja kwenu katika nguvu na dalili za Roho Mtakatifu; ili imani yenu isiwe katika hekima ama maarifa ya watu wa dunia hii, bali katika nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo; kwa sababu Yeye yu hai, yeye yule jana, leo, na hata milele." Mungu na atusaidie kuamini jambo lile lile, na Mungu athibitishe jambo lile lile kama vile Yeye amekuwa akifanya.

173 Yeye anakuzuia usione ufunuo wa kweli na imani ya Neno la Mungu likifunuliwa na kuthibitishwa leo, na shule zake, maktaba, vitabu, mahospitali, na kadhalika. Mnaona? Yeye anakuzuilia jambo hilo. Sasa anafasiri, kama alivyofanya kwa Farao, akijaribu kukufanya usione maana ya Neno lililothibitishwa la wakati Wake ulioahidiwa katika Nuru za jioni, zilizothibitishwa na kuhakikishwa. Yeye amejaribu, kwa maarifa yake, na mashule, na watu walioelimishwa vizuri zaidi, na maadili, na kadhalika, kukufanya usione jambo Hilo.

Cho chote kile, ili kwamba hutaangalia jambo Lile na kuona huyo ni Yesu Kristo! Unajuaje ni Yesu Kristo? Yeye ni Neno, Naye ni Neno la wakati huu. Na wakati huu, alisema ya kwamba jambo hili lingetukia katika wakati huu, na hili hapa likitukia. Mnaona? Mnaona? Yeye anajaribu awezavyo kukufanya msione jambo Hilo.

Atabandika jina lo lote chafu awezalo kwalo. Mnaona? Ataliita "mtakatifu afingirikaye" na cho chote kile. Yeye alimwita Yesu "Beelzebuli." "Nao wanamwita Bwana wa nyumba Beelzebuli, ni zaidi sana vipi watawaita wanafunzi?" Mnaona?

174 Mnaona, akijaribu kukufanya usione maana halisi ya Neno. Si yale. . . Mnaona, yeye analifasiri Hilo, akisema linamaanisha jambo *hili*.

Mungu alisema, "Niliahidi katika siku za mwisho ningewatumia Malaki 4." Halihitaji kufasiriwa; Yeye alilifasiri. Yeye alisema, "Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ulimwengu utakuwa katika hali ya Sodoma; na katika wakati huo, nitamfunua Mwana wa Adamu hiyo, kabisa." Tuna kila namna ya uigaji na kila kitu kingine, cha jambo hilo, bali tuna Mmoja halisi, pia. Mnaona? Yeye alisema angefanya jambo hilo.

Yeye alisema mpinga Kristo angeinuka na karibu awapoteze walio wateule kama yamkini. Lakini alisema, "Waache. Waache

waendelee. Upumbavu wao utadhihirishwa kwa watu wote." Kwa nini? Jaribio la Neno huhakikisha jambo hilo. Mnaona?

Inapofikia kwenye Neno, "Hilo lilikuwa nyuma *hivi*, *vile*? Loo! mimi siamini katika uzao wa nyoka. Siamini katika *hili*, *lile*, na lile *lingine*." Halijafunuliwa bado, mnaona, la, kamwe. Loo, ndugu, angalia tu ambapo . . .

Itatubidi kufunga, kwa sababu ni saa sita.

175 Angalia, anajaribu kukufanya usione maana ya Neno la wakati huu, ya Nuru ya jioni ikifasiriwa. Ni . . . Ina maana gani? Ni kwamba wakati wa kutoka umewadia, Mungu anakuja kumchukua, hakika kabisa. Mnaona?

176 Sasa nataka kuwauliza swali. Wakati, ni saa sita sasa, zimepita dakika tano baadaye; nasi tutaendelea, usiku wa leo. Mnamwona mungu wa wakati huu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini jambo hilo? ["Amina."] Mnaona jinsi ilivyo, kanisa, la kiakili, sayansi?

Ulimwengu mzima ni wake, mnaona, madhehebu. Na, unasema, mimi ni Mkristo. "Wewe ni wa madhehebu gani?" Vema, kama mimi nilikuwa mfuasi wa madhehebu, siamini ningekuwa Mkristo. Sasa, hilo ni Neno kubwa, lakini hilo ni kweli.

Ndiyo kwanza tu nimalize kusema ya kwamba maarifa na sayansi, na Ukristo, havina ushirika hata kidogo. Kimoja ni cha ibilisi, na hicho kingine ni cha Mungu. Cho chote kinachokana Neno la Mungu, jitenge nacho. Mnaona? La, bwana. Biblia inawahimiza Wakristo, kwa siku hizi za mwisho, watoke kwa kahaba huyo, huo ni mti wa kujua mema na mabaya.

177 Hakika, ana mambo mema. Je! mtu ye yote anaweza kusema mabaya juu ya hospitali? La, bwana. Maktaba? La, bwana. Elimu? La, bwana. Lakini, mnaona, wao wanawapa hayo bila ya Neno. Mnaona jinsi lilivyo danganyifu? Wanawapa kanisa la kuhudhuria, ibada ya kuabudu, "mungu aliyeketi kwenye kiti cha enzi." Biblia ilitabiri jambo hilo.

178 Sasa wewe ni mfuasi wa moja ya mashirika hayo. Kuna mawili tu ya hayo duniani sasa, daima imekuwa hivyo, na itakuwa hivyo mpaka Yesu atakapokuja, na moja ya hayo litaharibiwa. Sasa wewe ni mfuasi wa moja ya makundi hayo. Moja ya hayo, umejiunga nalo; hilo lingine, unazaliwa Kwake. Unaona?

Moja ya hayo, wewe ni sehemu yake kwa sababu umezaliwa ndani Yake. Huna budi kuwa sehemu Yake. Hivi ningeweza kukana nina mkono? Si zaidi ya vile ninavyoweza kukana Neno lo lote la Mungu, kama mimi ni sehemu ya Mungu. Mimi ni sehemu ya William Branham; niko katika sehemu mbalimbali, na kila sehemu ni sehemu yangu. Na kila Neno la Mungu halina budi kuafikiana na roho yangu, kuafikiana na nafsi yangu,

kuafikiana na maisha yangu, halina budi kuafikiana na mawazo yangu. Kama mawazo yangu ni kinyume Chake, basi Roho wa Mungu haishi ndani yangu. Hiyo ni kweli. Siwezi kukana Neno Lake moja.

179 Wewe ni mfuasi wa moja ya makundi hayo. Huna budi kuwa, haina budi kuwa. Aidha ni Mwili wa Mungu, ambao ni kwa Neno; ama mwili wa Shetani, kwa kanisa. Na ulimwengu mzima utalazimishwa kuwa mshiriki wa kanisa fulani; unaabudu mungu fulani. Huna budi kuabudu aidha mungu wa maarifa, unategemea yale unayosikia kwa maarifa, unategea *hili*, ama *lile*, ama *lingine*; ama unategemea Neno la Mungu, kwa imani, ukimtarajia Yeye alithibitishe na kulifanya kweli.

Kanisa halisi la Mungu linatazamia kuja kwa
ile siku ya ule Utawala wenye fahari wa Miaka elfu,
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakuja na kumchukua Bibi-arusi Wake anayengoja;
Loo, moyo wangu umejazwa na furaha nyingi ninapofanya kazi, kukesha na kuomba,
Kwa maana Bwana wetu anarudi duniani tena.

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Shetani atafungwa miaka elfu moja, hatutakuwa na majaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

180 Loo! watu wa Marekani hii, ambapo Ujumbe huu unaenda sasa, ukimbieni wakati huu tunaoishi wa maarifa na wa kisayansi upesi mwezavyo. Kimbilieni kwenye Neno la Mungu!

Ninyi, mimi, hakuna mtu ana—anayeweza kuthibitisha jambo Hilo; hakuna mtu awezaye kulihakikisha Hilo. Mungu huthibitisha Mwenyewe. Hakuna mtu aliye na haki ya kulifasiri Hilo; mimi, hakuna mtu mwingine aliye na haki. Mungu hujifasiria Mwenyewe. Yeye alitoa ahadi. Alisema angefanya jambo hili katika siku za mwisho.

Na katika siku za mwisho mungu wa wakati huu mwovu angeyapofusha macho ya watu, kwa maarifa yake ya kiakili, kwenye mti uliochanganyikana wa mema na mabaya, akiwa angali anawapa watu hayo. Na hapa inakuja, jambo hilo likiendelea, madhehebu hayo kutoka huko nyuma kabisa katika Nyakati za Giza, na kabla ya Nyakati za Giza, yote yakiishia kwenye mtu maalum, Shetani, aliyesema, “Nitajiinua nafsi yangu juu ya wana wa Mungu, nao watanisikiliza.” “Naye kama Mungu ataketi katika hekalu la Mungu, nao wana wa Mungu watalipenda sana.”

181 Mbona, mwana wa Mungu, anasema, “Vema, mke wangu, si ninii; yeye ni mzuri . . . ” Endelea, endelea tu. Mnaona?

Unasema, “Vema, Yeye alisema ‘wana wa Mungu.’” Naam, bwana.

Mwanamume, hata awe nani, alifanywa kwa sura ya Mungu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Na mwanamke ni kitu kilichotolewa kwa mwanamume, si kwa Mungu. Kweli. “Wakati wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu ni wazuri, wakajitwalia wake.”

“Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku Zake Mwana wa Adamu.”

Sasa angalia, ukitaka kujua kanisa liko kwenye kiwango kipi, angalia wanawake wako kwenye kiwango kipi, unaona, maana mwanamke ni kanisa. Angalia yale anayofanya, unaona, na katika wakati huu mwovu wa kikahaba.

182 Angalieni, hakukuweko na mji mchoyo zaidi, mwovu zaidi, ulio duni sana na wa kikahaba kuliko Nazareti, na kutoka mle Mungu akamchagua bikira. “Jambo jema lingeweza kutoka Nazareti?”

Na kutoka katika wakati huu mwovu, ambapo mungu wa wakati huu ameyapofusha macho ya watu, kwa mafundisho yao ya sharti na madhehebu; kutoka kwenye wakati uo huo, Mungu anawachagua watu kwa ajili ya Jina Lake.

Ingawa hapa wanadharauliwa na kutwezwa, siku moja Bwana atawaleta
Wateule wake ndani ya lango, na hilo linastahili kila kitu.
Ndipo tutaimba na kupaza sauti, na kucheza kila mahali,
Mwana-Kondoo atayafuta machozi yetu;
Tutakuwa na juma moja la kurudi nyumbani,
Miaka elfu kumi ya kwanza. (Hiyo ni kweli.)

Watu wa ajabu sana kwa ajili ya Jina Lake nao wanaitwa Bibi-arusi Wake. (Hiyo ni kweli?)
Ingawa wanadharauliwa na kutwezwa, siku moja Bwana atawaleta
Hao waliochaguliwa ndani ya lango, (katika kule kutoka) na hilo linastahili kila kitu kwangu.

183 Ninakuwa mzee. Na siku zangu zinaanza kwisha; na macho yangu yanaanza kufifia; na mwali wangu wa maisha unaanza kufifia. Mimi siogopi giza. Kwa maana nataka kusema jambo hili, pamoja na Paul, “Ninamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake.” Haidhuru watanizika wapi, kama nikizama baharini, ama nikiungua kwenye tanuru, ama kuliwa na simba, Yeye ataliita jina langu, nami nitanena. Amina!

Na tuombe.

184 Kama yupo hapa, ama huko nje kwenye simu za huu Ujumbe kila mahali nchini, katika makanisa yenu madogo na makundi na kwenye kumbi, na po pote mnapoketi, kama kuna mmoja,

loo! hebu nikushawishi; hebu nikusihi, kama mhudumu wa Injili; hebu nikusihi, katika Jina la Yesu Kristo; itoroke hasira ya wakati huu mwovu! Usimtumikie mungu wa wakati huu mwovu.

Loo! ninajua ya kwamba unasema, "Ni kitu kizuri. Hayo ni sawa." Hakika, mti ulichanganyikana. Huwezi kuchanganya maarifa pamoja na Neno la Mungu.

Ni Neno linalopaswa kuaminiwa kwa imani, si maarifa. Hulielewi; wewe likubali. Unasema ni kweli, kisha unaishi Kwalo. Hilo ndilo tu analokusihi ufanye.

Kama kuna ye yote aliyeko hapa katika kikundi chetu, hatuwezi kufanya mstari wa maombi kuwaleta hapa, kwa maana hakuna nafasi; ama huko nje hewani, huko kwenye simu, kama kuna mtu huko asiyemjua Yeye. Usininii . . .

185 Loo, enyi wanawake, nimewakemea asubuhi ya leo, si mimi, nimenukuu tu Neno. Nywele fupi, kuvaa maskini hizo nguo fupi, kuvaa uonekane kizinifu kweli kweli, hivi hutambui ya kwamba roho huyo ambaye . . . Unaweza ukawa msafi, dada, mpenzi, inapofikia mwili wako, bali katika nafsi yako hivi huoni ni nini kimekushika?

Je! Mungu angemfanya binti Yake kuonekana mzinifu kusudi amdanganye mwanawe mwenyewe, kumtamani, kuwafanya wote wawili wawajibike kwa ajili ya uzinzi? Hivi Yeye angeweza kufanya jambo hilo, dada? Jiulize swali hilo. La, si kwa maili milioni kumi. Usimlaumu Mungu kwa jambo hilo.

186 Ndugu, hivi mungu amekupa roho ya ulimwengu huu hata huwezi kuona ya kwamba jambo hilo ni kosa? Hivi Yeye amepofusha macho yako, kwa maadili ya kanisa, madhehebu, kanuni za imani, na kadhalika, hata huwezi kuona ya kwamba Mungu anathibitisha Neno Lake na kulifanya ni kweli? Hivi kazi yako, tajiri wako, mke wako, watoto wako, kanisa lako, ama cho chote, vimekutenganisha na Neno la Mungu, ambalo ndilo chanzo pekee cha Uzima? Ikimbie, ndugu yangu. Ninakupenda, kwa upendo wa kiungu. Mimi siheshimu ye yote wa ndugu zangu zaidi yako, hata kidogo. Kama niliwaheshimu zaidi, ningeonyesha upendeleo. Sisemi mambo haya kukufanya ukasirike. Ninaonyesha, ninasema mambo haya kwa sababu yako kwenye Neno la Mungu. Na kama mtumishi wa Mungu, na upendo wa Mungu moyoni mwangu, ninawaambia mambo hayo ili kwamba mwone na mfahamu. Labda hamngeyejua kama sikuwaambia. Mtaikimbia leo?

Sasa, na kila mahali nchini, na tuinamishe vichwa vyetu.

187 Mungu mpenzi, mbele yangu kuna leso. Watu ni wagonjwa; ninaweka mikono yangu juu yazo, kusudi uwaponye.

188 Nami ninatumaini, Bwana, usiku wa leo, ya kwamba kutakuweko na ibada kubwa, ya kwamba Nguvu za Mungu

zitakuweko hapa, ishara kuu na maajabu. Kama tulivyosikia matokeo kutoka kwenye mikutano hii michache iliyopita, ni ajabu jinsi gani, kuona yaliyotukia! Ninaomba, Mungu mpenzi, ya kwamba Wewe utatupa sehemu maradufu usiku wa leo. Ninaomba kwa moyo mnyofu, Bwana, kwa sababu ni upendo wangu Kwako na kwa Neno Lako, na kwa ajili ya watu hawa. Tujalie, Mungu mpenzi.

189 Na endapo huko nje kila mahali nchini, ama hata hapa sasa, ya kwamba kuna wengine walio wagonjwa na wanaoteseka, na hawana budi kwenda usiku wa leo, hawatakuwa hapa, ama watakuwa huko nje katika makanisa na mahali ambapo wamekusanyikia; ninakuomba Wewe uwaponye. Sasa, Bwana, lakini kwa kuponya kukuu kuliko kote! Kama ukiponya miili yao ya kawaida kutokana na kansa, TB, niumonia, kitu fulani, wao watakuwa wagonjwa tena, hapana shaka, kama wakiishi muda mrefu sana, kwa maana mwili wao ungali chini ya dhambi, lile laana. Lakini hebu wao wapate kuponywa Kiungu ha—halisi, kuponywa kwa nafsi, ambako kunafanya kiumbe kipya, kinachopita mautini kuingia Uzimani, halafu kinangojea kwenye maskani haya ya kale ukombozi wa mwili baada ya nafsi kukombolewa. Tujalie, Bwana.

190 Naomba wayakimbie hayo madhehebu na kanuni za imani. Mungu, huko ndani kabisa ya hizo kanuni za imani na madhehebu nimekutana na baadhi ya ndugu walio wazuri sana. Na, Mungu, ninaweza kusema jambo hilo vipi wapate kuona, na kuwafanya walione Neno? Linanitatiza. Lakini ninajua, tena, ya kwamba Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja," hata awe mzuri jinsi gani, jinsi alivyo mnyenyekevu, mpole, "asipoitwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watakuja." Na, Bwana, ninajisikia nikiwajibika kusema Kweli.

Na si kama alivyosema Paulo, "Kulichanganya Neno la Mungu na uongo," pamoja na mafundisho ya sharti ya madhehebu yamechanganywa ndani Yake, kama mti wa mchanganyiko wa mema na maarifa, mema na mabaya; bali tukiwa na moyo mkunjufu pamoja na Roho Mtakatifu. Tujalie, Mungu. Mwokoe kila mtu.

191 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa na macho yetu yamefungwa. Na si kwa mimi . . . Siwezi kulisema namna hii, "Haileti tofauti kwangu kama utafanya ama hutafanya." Inaleta tofauti kwangu. Ninawapenda. Nami natumaini hamfikiri kwa maana inanibidi kuzungumza kwa ukali . . . Kama Paulo alivyosema, "Ningekuwapo pamoja nanyi sasa, ningebadilisha msimamo wangu." Haikuwa ni kwa sababu yeye hakuwapenda; aliwapenda. Si . . .Kwa kuwa ilimbidi Yesu kuwakemea, halafu awafie. Mnaona, "Baba, wasamehe; hata hawajui watendalo." Kuwazia, binadamu anayetaka kuwa sahihi, na kujaribu kuwa sahihi, na kumwona yule ibilisi . . .Huyo ndiye ninayempinga, ambaye ameyapofusha macho ya watu hawa.

192 Taifa hili linapaswa kuwa likiwaka kwa utukufu wa Mungu, kuona yale yametokea ndani yake katika siku hii ya mwisho, hii ya mwisho. Kwa nini ufufuo huu haujashika nchi za zamani? Hii ni Pwani ya Magharibi huku, magharibi ya mbali sana uwezayo kwenda. Sasa kizuizi cha dhambi kimenguruma chini ya dunia, nayo inazama; mahali, na Los Angeles na Hollywood, inazama inchi kadha kwa saa, hakuna njia ya kuzuia jambo hilo. Naam, tumefika. Karibu wakati wo wote tutasikia ule wito. Kama unajua jambo hilo. . .

Sasa, mtu ye yote asiangalie. Lakini iwapo unajua, kutoka moyoni mwako. . .ninakuuliza. Siwezi kujua moyo wako, isipokuwa Mungu aufunue. Lakini kutoka moyoni mwako, kama unaweza kuona ya kwamba wewe huko mahali unapopaswa kuwa na Mungu na Neno Lake, katika imani, je! waweza tu kumwinulia mkono wako, umwambie, "Bwana, nisaidie." Ee Mungu! Kutoka katika kanisa hili, limejaa, limejaa kila mahali kuzunguka kuta, ndani na nje, kwa kweli mamia ya mikono, labda mikono mia mbili iliinuliwa. Asanteni kwa uaminifu wenu.

193 Mpenzi Yesu, usiache mmoja wao apotee. Kama mtumishi Wako, anayesimama kati ya walio hai na waliokufa, akiwaelekeza, kwa kidole, kwenye Neno la Mungu. Siwezi kuwaokoa, Bwana, lakini wao wanataka kuokolewa. Na, Baba, kama nilivyosema mara nyingi, jua huchomoza asubuhi; na linapokuja kupitia duniani, limetumwa na Mungu kuivisha nafaka, kutengeneza chakula cha kawaida kwa maisha ya kawaida. Lakini, Ee Mungu, Wewe ulisema, "Kwao walichao Jina Lake Jua la haki litazuka lenye kuponya katika mbawa Zake." Jalia Jua la haki, Neno la Mungu, lizuke mioyoni mwa watu, na miali ya imani iponyayo katika hilo Neno iponye kila kutotii kwa Neno, na kuwaleta kufikia utimilifu wa wana na binti za Mungu.

Wao ni Wako, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, hapa na huko hewani pia, ninawakabidhi hao walioinua mikono yao Kwako kwa ajili ya wokovu wa nafsi zao. Amina.

> Humu nitapumzika (Wapi? Madhababuni.)
> Mahali pa raha. . .(kwa imani ninaangalia kule ng'ambo ninakokwenda)
>
> Msalaba, (hapo ndipo Neno linaponing'inia)
> . . .Msalaba,
> Humu nina sifa;
> Hata nitapumzika
> Mahali pa raha.
>
> Yesu unihifadhi. . .(Hiyo ni kusema, kusulubishwa pamoja Naye, sitaki

kitu cha ulimwengu. "Niweke huku nimesulubishwa.")
Hapa msalabani,
Wajiao Kalvari,
Waponye damuni.

Msalaba, msalaba,
Humu nina (hebu tuinue mikono yetu) sifa;
Hata nitapumzika
Mahali pa raha.

194 [Ndugu Branham anazungumza sasa na wana muziki—Mh.] "Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita."

Nyosha mkono na kuushika mkono wa mtu fulani, na kusema, "Mungu akubariki, ewe Mkristo."

[Ndugu Branham anazungumza tena na wana muziki—Mh.] Ninaweza kumsikia Mwokozi Wangu akiita."

Mnauhisi Uwepo Wake? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Huko nje kwenye mawimbi ya simu, nyote peaneni mikono huko nje, na kusema, "Mungu akubariki, ewe Mkristo."

195 Mnajua, kuna kidimbwi cha maji huku nyuma. Yeye anawachukua watu wanaovaa Jina Lake. Hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo upate ondoleo la dhambi zako, kuna kidimbwi, kuna majoho, kuna mtu anayesimama akiwa tayari. Mnakaribishwa, kama kweli unamkubali Yesu kama Mwokozi wako na kuamini ya kwamba hiyo ni Kweli.

196 Kumbukeni, hakukuweko kamwe na mtu katika Biblia, ama wakati wo wote kabla ya kuundwa kwa madhehebu ya kanisa Katoliki, aliyepata kubatizwa kwa njia nyingine yo yote ila katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Hakuna mahali panapopatikana katika Maandiko, ama historia, ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa, katika Kanisa la Mungu aliye hai, katika jina la vyeo vya "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ni fundisho la sharti la Kikatoliki, wala si fundisho la Biblia.

197 Nilipokuwa nikihojiwa na kasisi fulani, nilimwuliza jambo hilo. Akasema, "Hiyo ni kweli. Lakini sisi ndio kanisa; tunaweza kubadilisha lo lote tutakalo. Uchaji uko katika kanisa. Mungu yuko katika kanisa Lake."

198 Nikasema, "Mungu yuko katika Neno Lake. Na kama kanisa ni . . ." Nikasema, "Mungu ni Neno. Na iwapo kanisa linapingana na Neno, basi mimi siamini kanisa."

Ninaliacha kila neno la mtu liwe uongo, kama ni kasisi, papa, ye yote yule, na Neno la Mungu liwe kweli.

Naye Paulo alimfanya kila mtu, haidhuru alikuwa amebatizwaje, kama hakuwa amebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, aje abatizwe tena.

199 Na baada ya wengine kupokea Roho Mtakatifu, Petro alisema, "Tunaweza kukataza maji, kwa kuwa hawa wamepokea Roho Mtakatifu," Matendo 10:49, "kwa kuwa hawa wamempokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi hapo mwanzo?" Naye akawaamuru, "Kabla hamjaondoka mahali hapa, ingawa mmempokea Roho Mtakatifu, njoni mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo."

Kwa kuwa, Petro alipewa ufunguo wa Ufalme, akisema, "Lo lote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni." Na ufunguo hufanya nini? Unafungua kitu fulani, siri.

200 Na wakati Yesu aliposema, "Enendeni, mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," akiweka hilo hapo kuwapofusha wasioamini.

Angalia! Kwa nini Petro hakutimiza jambo hilo, neno kwa neno? Ilimpasa kufanya jambo hilo.

Kama mtu amebatizwa katika vyeo, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," yeye hajabatizwa kamwe; hana Jina. *Baba* si jina, *Mwana* si jina, na *Roho Mtakatifu* si jina. Roho Mtakatifu ni kile alicho Yeye; kama vile, mimi ni mwanadamu. Ni Roho Mtakatifu.

*Baba* ni cheo; mimi ni baba. *Mwana* ni cheo; mimi ni mwana. *Mwanadamu* ni cheo; hivyo ndivyo nilivyo. Lakini jina langu ni William Branham.

Nalo Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu ni Jina la "Yesu Kristo." Yesu alisema, "Nimekuja katika Jina la Baba Yangu." Jina la Baba ni lipi? Mwana ye yote huja katika jina la baba yake. Nalo Jina la Baba ni Yesu Kristo. Mnaona? Mnaona ninalomaanisha?

201 Kama nilikwambia ushuke uende ukaniletee kitu fulani kutoka kwenye kaunta hapa chini, katika jina la meya wa mji. Ni wangapi wanajua jina la meya wa mji ni nani? Rafiki yangu mwema, Rich Vissing. Vema, hungeenda kule chini na kusema "katika jina la meya wa mji." Unasema, "Katika jina la Richard Vissing." Ninyi watu wa hapa Jeffersonville mnajua yeye ni nani.

Na hiyo ndiyo sababu Yeye alisema Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ndani Yake mnakaa Uungu, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Alisema, "Wabatizeni katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

202 Petro akisimama pale akiwa na ufunuo ambao Yeye alijenga Kanisa Lake, wa Yeye alikuwa ni Nani, alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Na kamwe. . .Funguo zilizungushwa Mbinguni na duniani. "Hakuna Jina lingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa."

203 Kwa nini mnabatiza katika Jina la Yesu Kristo? Kwa ondoleo la dhambi. "Kila mtakayemwondolea dhambi, zimeondolewa."

Mnaona? Lakini kama hufikiri yeye anastahili na anafaa kubatizwa, usimbatize. Kwa kuwa, unapofanya jambo hilo, hilo linafanyu hivyo, mnaona. Mnafahamu ninalomaanisha?

> Ninaweza kumsikia Mwo- . . . (Neno) akiita,
> (akiita kule chini kaburini)
> Ninaweza . . . ("Je! hutakufa pamoja Nami,
> kusudi upate kufufuka pamoja Nami?") . . . -
> kozi akiita,
> Ninaweza kusikia Mwokozi wangu akiita,
> (ulimwengu utasema nini?)
> "Utwae msalaba wako, unifuate, unifuate . . . "

Sasa, kama hujaninii:

> Aniongozapo (Yeye ni Neno) . . . (pale kuna
> kidimbwi)
> Aniongozapo nitafuata,
> Aniongozapo nitafuata,
> Nitaambatana Naye, Naye kote.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

204 Mungu mpenzi, kidimbwi kiko tayari. Sasa nena na mioyo yetu, Bwana. Naomba wamsikie Kristo, lile Neno, likiwaita, na waambatane Naye kote.

"Nitaambatana Naye shambani. Nitaambatana Naye kwenye kidimbwi. Nitalichukua Jina Lake. Ninataka kuwa mmoja wa watu anaowaita kwa ajili ya Jina Lake. Nitaamini Neno Lake. Nitafuata. Sitabembana na ulimwengu. Nitakuwa Bibi-arusi mwaminifu, aliyeposwa. Sitaacha nukta moja ya Neno Lake. Kila haja, nitakuwa Bibi-arusi halisi, wa kweli. Kila analoniomba kufanya, nitalifanya.

"Kama Mume wangu anayekuja anataka niache nywele zangu zikue, nitafanya jambo hilo. Kama anataka niondoe vipodozi hivi vyote, nitafanya hivyo. Kama anataka . . . Akiniambia ni pepo mchafu, yule mwovu ninayebembana naye, nikiwa na nguo hizi zinazoonekana ni za kizinifu; nitafanya hilo, nitazitoa. Sijali mtu mwingine ye yote anasema nini, nitazitoa.

"Akitaka nitoke kwenye kundi hilo nililomo, la wasioamini, nitafanya hilo; ingawa nitaoka mkate wangu, ama cho chote kile. Yeye aliahidi hataniacha wala kunipungukia. Nita—nitafanya hivyo. Nitaambatana Naye kote. Ananitaka nibatizwe katika Jina Lake, nitabatizwa."

Bwana, Wewe uliahidi jambo hilo katika Neno Lako hapa, hivyo ndivyo ulivyotaka. Jalia kila mtu aone jambo hilo, Bwana, na alikubali kwa unyenyekevu na utamu. Katika Jina la Yesu naomba. Amina.

205 Ninyi ni mali ya Mungu. Naomba Mungu ayachukue hayo maneno madogo yaliyovunjika-vunjika na kuyafanya halisi kwenu, ndilo ombi langu nyofu.

Kidimbwi kitakuwa tayari. Mtu ye yote anayetaka kuja, wana. . .Mhudumu atatangaza hilo baadaye kidogo. Ye yote ambaye ametubu na anataka kubatizwa, kwa kutumia Jina la Yesu Kristo, wewe njoo moja kwa moja. Kila kitu kiko tayari. "Mombo yote yako tayari." Kila kitu ambacho tunaweza kufanya kukusaidia kumwishia Mungu, tuko hapa kufanya jambo hilo. Mungu awabariki.

206 Sasa hebu tusimame. Sasa ule wimbo wetu mdogo, *Nampenda*, "Nampenda kwa sababu Yeye alinipenda kwanza." Hebu tuuimbe, kila mtu sasa.

Nampenda, (na tuinue mikono yetu tunapouimba)
Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa sasa, na tumvumishie huo. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

Nampenda.

[Ndugu Branham anaendelea kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

Ee Mungu, Baba yetu, turehemu sisi viumbe maskini, Bwana. Tutie nguvu kwa ajili ya kazi iliyo mbele zetu. Nisaidie, Ee Mungu, nisaidie! Ninaona kwamba kitu fulani kiko papa hapa, Baba. Nisaidie, Ee Mungu, kujua Kweli. Wabariki watu hawa, Mungu mpenzi. Waongoze, naomba, katika Jina la Yesu.

207 Sasa wakati tunapoinamisha vichwa vyetu, nitamwomba mchungaji hapa, Ndugu Neville, ndugu yetu mpendwa, aje papa hapa sasa na kusema anayotaka kusema, habari za. . . kuhusu ubatizo. Huenda nikatangaza jambo hilo. Nafikiri kidimbwi kimefunguliwa, hata hivyo.

*Mungu Wa Wakati Huu Mwovu* SWA65-0801M
(The God Of This Evil Age)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 1 Agosti, 1965, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2004 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org